BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT
1,014,872,576/-
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#



UKURASA 3

**CCM** yatoa neno mikopo wanafunzi wa elimu ya juu



RAYVANNY HUYOOO! NANI KUFUATA NJIA YAKE?

UKURASA 11


# Nipashe

Jumamosi Julai 16, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581008

www.ippmedia.com


www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper


# Utouh alia tril. 1.2/- kutoonekana Hazina

UKURASA 2



Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Bajeti, Daniel Sillo (katikati), Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya WAJIBU, CAG mstaafu Ludovick Utouh (kushoto) na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa taasisi hiyo, Yona Killagane, wakionyesha Ripoti ya Uwajibikaji ya Mwaka 2020/21 iliyoandaliwa na taasisi hiyo, baada ya kuizindua, jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri Mkuu abaini ufisadi stendi mabasi

UKURASA 2



## Mama, mwana kortini madai mauaji ya ndugu

UKURASA 3

**MICHEZO** | **SIMBA: TUTAFANYA MAKUBWA, TULIENI** UK.24 | **MAONI, KATUNI** UK.6

# Waziri Mkuu abaini ufisadi stendi mabasi

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amebaini ufisadi wa mamilioni ya shilingi katika Kituo Kikuu cha Mabasi cha Manyoni mkoani Singida baada ya mawakala kutokufikisha fedha katika Halmashauri ya Wilaya.

Kutokana na kubaini hilo, ameiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuwakamata na kuwahoji watu wanne wanaodaiwa kuwa ni mawakala waliopewa kazi ya kukusanya mapato katika kituo hicho.

Ametoa agizo hilo jana wakati akizungumza na watumishi wilayani Manyoni na kuwataka watu hao alioagiza wasakwe na kukamatwa kuwa ni Mussa Chacha, Mathias Shija na wengine aliowataja kwa jina moja ambao ni Justine na Leya.

Alisema watu hao walipewa kazi ya kukusanya mapato ya halmashauri lakini kiwango cha fedha kilichokuwa kinapelekwa ni kidogo kulinganisha na mapato halisi yaliyokuwa yanakusanywa.

Majaliwa alisema katika kituo cha Manyoni, zaidi ya mabasi 200 yanaingia na kila moja hutozwa Sh. 2,500 na kwa magari madogo 1,500 lakini kiasi cha fedha kinachopelekwa kwenye halmashauri kwa mwezi ni Sh. 1,786,000 tu.

"DED (Mkurugenzi Mtendaji) unamjua Musa Chacha ni mtumishi wa umma ni wakala lakini mmempa kazi ya kukusanya ushuru wa stendi, hali hii ndiyo inasababisha mapato tunayopata kuwa kidogo," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Melkzedeck Humbe, alipoulizwa kuhusu Chacha, alisema si mtumishi wa umma ni wakala anayefanya kazi ya kukusanya ushuru.

Katika maelezo yake, mkurugenzi huyo alijichanganya na kusema kuwa kila basi linaloingia stendi hutozwa Sh.3000 na kusahihishwa na Mweka Hazina ambaye alitaja kiwango sahihi ni Sh.2,500.

"DED mabasi yanatozwa shilingi ngapi? Elfu tatu Mkuu, huyu hajui, Mweka Hazina jibu," ndipo alipotaja Sh.2,500 kwa mabasi na magari madogo Sh.1,500.

Majaliwa alisema baada ya kubaini kuna ujanja katika ukusanyaji wa mapato kwenye stendi, serikali ilimuweka mtu wake, Anderson Kamugisha ambaye katika kipindi cha wiki mbili alikusanya Sh. 2,077,000 ikilinganishwa na Sh.1,786,000 zilizokusanywa na wakala aliyewekwa na halmashauri.

"TAKUKURU nawaagiza muwahoji wote, mkiacha huyo tuliyemuweka sisi (Kamugisha), tujue nani aliwapa kazi hiyo ya kukusanya ushuru ili hatua zichukuliwe," aliagiza.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akikagua mradi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mkoa wa Singida, katika kata ya Solya, Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni jana. **PICHA: OWM**

Waziri Mkuu aliongeza kuwa na kikundi cha wakusanya mapato watatu ambao ni miongoni mwa watakaohojiwa ambao walipewa 'fosi' moja wakakusanya kwa miezi mitatu Sh. milioni 38 tu.

Alisema baada ya serikali kubaini kulikuwa na ujanjaujanja alipewa mtu mwingine fosi moja ambaye alikusanya Sh. milioni 21.8 kwa mwezi mmoja wakati kikundi cha wakusanya mapato kilikusanya Sh. milioni 38 kwa miezi mitatu.

Majaliwa alisema katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni kumekuwa na ufujaji wa fedha ambapo zinazokusanywa kwenye vyanzo vya mapato hazipelekwi badala yake zinaishia kwa watu.

Alisema serikali haitakubali kuona hali hiyo ikiendelea na hivyo hatua zitachukuliwa kwa wahusika.

Waziri Mkuu anaendelea na ziara ya siku tano mkoani Singida ya kukagua miradi ya maendeleo.

# Utouh alia na tril 1.2/- kutoonekana Hazina

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MKURUGENZI wa Taasisi ya WAJIBU, Ludovick Utouh, ameishauri serikali kuhakikisha fedha zote inazozikusanya, zipite kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Katiba.

Vilevile, ameishauri serikali kuwawajibisha maofisa wote waliotajwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusika katika kashfa ya uteketezaji wa noti halali za Sh. bilioni 3.9 kwenye Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ili kuchochea uwajibikaji na utawala bora.

Utouh aliyewahi kuwa CAG mwaka 2006 hadi 2014, alitoa rai hiyo jana jijini hapa wakati wa uzinduzi wa Ripoti ya Uwajibikaji ya Mwaka 2020/21 iliyoandaliwa na Taasisi ya WAJIBU kutokana na uchambuzi wa ripoti ya CAG kwa mwaka huo wa fedha.

Alisema Ibara ya 135 ya Katiba inataka fedha zote zinazokusanywa na serikali zipite kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali isipokuwa fedha zilizoamuliwa kwa mujibu wa sheria kupelekwa moja kwa moja kwenye miradi.

Alisema ripoti ya CAG kwa mwaka 2020/21 inaonyesha Sh. trilioni 1.254 zilizokusanywa na serikali, hazikuingizwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

"Hatumaanishi fedha hizi zimeliwa au zimeibwa, lakini hazionekani kwenye mfumo wa serikali. Wizara ya Fedha itafute utaratibu wa kuzipitisha fedha hizo kwenye mfumo unaotakiwa," alishauri Utouh.

Kwa kurejea ripoti yake ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu kwa mwaka 2020/21, CAG Charles Kichere, anabainisha namna ulivyo usuluhisho wa fedha zilizokusanywa na fedha zilizowasilishwa Mfuko Mkuu.

Anasema usuluhisho huo unaonyesha kuwa kwa mwaka wa fedha 2020/21, serikali ilikusanya Sh. trilioni 31.326 sawa na asilimia 89.8 ya makadirio yaliyoidhinishwa ya Sh. trilioni 34.879, hivyo makusanyo ya Sh. trilioni 3.553 (asilimia 10.19) hayakukusanywa.

CAG anafafanua zaidi kuwa kati ya makusanyo yote, Sh. trilioni 30.072 zilipokewa Mfuko Mkuu wa Hazina, hivyo kufanya utofauti wa Sh. trilioni 1.254.

**BOT, TPA**

Nipashe ilipotaka kujua jambo lililomshtua zaidi katika ripoti ya CAG kwa mwaka 2020/21, Utouh alitaja mambo mawili ambayo ni hasara ya mabilioni katika mradi wa uongezaji kina cha Bandari ya Tanga na kashfa ya uteketezaji wa noti zenye thamani ya Sh. bilioni 3.99 uliofanywa na maofisa wa BoT kinyume cha taratibu.

"Kuna vitu vinapaswa kushughulikiwa kwa nguvu kubwa pindi vinaporipotiwa na CAG na wananchi waone hatua zinazochukuliwa. Serikali ichukue hatua dhidi ya watendaji waliotajwa katika mambo haya ya Bandari ya Tanga na uteketezaji wa noti za BoT," alishauri.

**NOTI ZA BOT**

Kwa kurejea ripoti yake ya kwa mwaka 2020/21, CAG Kichere anasema alibaini tatizo alipokuwa anafuatilia tuhuma za ubadhirifu wa noti chakavu uliofanyika BoT kuanzia Januari 2017 hadi Desemba 2019.

Anasema alifanya ukaguzi maalum BoT baada ya ofisi yake kuombwa na Naibu Gavana (Utawala na Udhibiti wa Ndani) kufanya ukaguzi wa kiuchunguzi.

"Lengo la ukaguzi wangu lilikuwa ni kujua kiasi cha hasara ambacho Benki Kuu ilipata na watu waliohusika katika ubadhirifu huo. Kupitia uchunguzi wangu, nilibaini Benki Kuu ilipata hasara ya Sh. bilioni 3.99 kwenye urejeshaji wa noti chakavu.

"Kulingana na sera na miongozo ya Benki Kuu, noti chakavu ni noti halisi yenye kukosa sifa za kufanya malipo halali. Benki Kuu ina mamlaka ya kupokea na kurejesha thamani ya noti mbovu (chakavu) na kutoa noti mpya," anasema.

CAG anafafanua kuwa katika ukaguzi wake, alibaini BoT ilipokea noti za Sh. bilioni 4.17 ambazo ni noti 417,006 za Sh. 10,000 kati ya Januari 2019 hadi Septemba 2019, ambazo zilidaiwa kuwa ni chakavu ili zibadilishwe na kutolewa noti mpya.

Anasema katika uchunguzi wake, alibaini kuwa noti 1,427 zenye thamani ya Sh. milioni 14.27 zilikuwa safi na zinafaa na hivyo hazikuwa na sifa ya kuwa noti chakavu.

Pia alibaini kuwa noti 16,187 zenye thamani ya Sh. milioni 161.87 zilikidhi vigezo vya kurejeshwa BoT na kutolewa noti mpya, wakati noti 399,392 zilizobaki zenye thamani ya Sh. bilioni 3.99 hazikuwa na vigezo vya kupewa noti mpya na zilipewa noti mpya kwa njia ya udanganyifu uliofanywa na maofisa wawili na watunza fedha wanne wa BoT.

**BANDARI YA TANGA**

Kuhusu kilichomshtua Utouh kwenye Bandari ya Tanga, CAG Kichere anasema alibaini mkandarasi aliyepewa kazi ya kuongeza kina cha bandari hiyo na Mamlaka ya Bandari (TPA), alimpa kazi hiyo mkandarasi mwingine bila kutoa taarifa kwa mamlaka.

Vilevile, CAG alibaini kufanyika malipo zaidi ya gharama halisi za mradi huo kwa Sh. bilioni 64.3, akipendekeza serikali ichukue hatua stahiki dhidi ya wahusika.

CAG Kichere anafafanua kuwa TPA iliingia mkataba na mkandarasi mkuu wa Sh. bilioni 172.36 Agosti 3, 2019 wa muda wa mwaka mmoja hadi kufikia mwezi Agosti 2020 kwa ajili ya kuongeza kina cha lango na sehemu ya kugeuzia meli katika Bandari ya Tanga.

Anabainisha kuwa mkataba huo pia ulijumuisha kufanya tathmini ya athari za kimazingira na kununua vifaa kwa ajili ya shughuli za bandari.

CAG anasema kuwa kulingana na mkataba, gharama ya kuongeza kina cha lango na sehemu ya kugeuzia meli katika Bandari ya Tanga ilikuwa ni Sh. bilioni 104.92 (asilimia 60 ya bei yote ya mkataba).

Hata hivyo, CAG anabainisha kuwa mnamo Agosti Mosi 2019, mkandarasi mkuu iliingia makubaliano na mkandarasi mbia kwa ajili ya kazi ya kuongeza kina cha lango na sehemu ya kugeuzia meli kwa bei ya mkataba dola za Marekani milioni 18.15, sawa na Sh. bilioni 40.46 kwa kipindi cha miezi 11 bila kutoa taarifa kwa TPA.

Katika uzinduzi wa Ripoti ya Uwajibikaji jana, Mweyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti Daniel Sillo, alitoa rai kwa WAJIBU kushiriki kutoa maoni katika marekebisho ya sheria mbalimbali ikiwamo ya ununuzi na maboresho ya Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Japhet Hasunga, alishauri kupunguzwe muda wa taasisi kuwasilisha taarifa ya fedha kutoka miezi mitatu ya sasa hadi mwezi mmoja, pia CAG apunguze muda wa kuandaa ripoti kutoka miezi sita ya sasa, ili mjadala ufanyike kwa wakati.

Hafla ya uzinduzi huo ilihudhuriwa na viongozi wa taasisi mbalimbali za serikali na zisizo za kiserikali zikiwamo TAKUKURU, HakiElimu, Sikika, TRA, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, TMF, NAOT, TGNP, FCS, Bodi ya Taifa ya Uhasibu na Msajili wa Hazina.

## HABARI KITAIFA



Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka (wa pili kushoto) akisalimiana na Mkazi wa jimbo la Gando, visiwani Pemba jana, baada ya kumkabidhi baiskeli ya kutembelea iliyotolewa na Mbunge wa jimbo hilo, Salim Mussa Omari (wa pili kulia). Kulia ni Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kaskazini Pemba, Mberwa Hamad Mberwa. **PICHA: FAHADI SIRAJI WA CCM**

# Mama, mtoto kortini mauaji ya ndugu

**Na Grace Gurisha**

MAMA na mtoto wake wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, kwa madai ya kumuua Beatrice Magombola ambaye ni ndugu yao wa damu moja.

Washitakiwa hao ni Alphonse Magombola (34) mkazi wa Bunju B Mpakani na Sophia Mwenda (61) mkazi wa Mbagala, Dar es Salaam.

Marehemu Beatrice na Alphonse ni mtu na mdogo wake na Mwenda ni mama yao mzazi.

Akisoma hati ya mashitaka, Wakili wa Serikali Faraja Ngukah alidai jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Ritha Tarimo kuwa watu hao wanashtakiwa kwa mauaji ya ndugu yao.

Ngukah alidai kuwa washtakiwa hao Desemba Mosi, 2020 wakiwa eneo la Kijichi ndani ya Temeke, Dar es Salaam, walimuua Beatrice Magombola.

Baada ya washtakiwa hao kusomewa shitaka lao, mshtakiwa wa kwanza alidai kuwa kwamba kutokana na mateso ya muda mrefu kuanzia Machi 17,2022 na kuendelea, aliumia mguu wake wa kulia.

"Kutokana na kupigwa kwa muda mrefu mguu wangu wa kulia umepata hitilafu. Naomba nipatiwe matibabu," alidai Alphonse.

Hakimu Tarimo alimweleza Wakili Ngukah kama amesikia alichokidai Alphonce na kujibu kwamba amesikia na kueleza kwamba huko mahabusu (Magereza) atakakopelekwa kuna matibabu, kwa hiyo atapata huduma hiyo na kama shida yake ni kubwa atapelekwa hospitali ya rufani. Baada ya maelezo hayo, Hakimu alimhoji Alphonse kama ifuatavyo;-

**Hakimu:** Umesema toka lini upo mahabusu?

**Alphonsce:** Tangu Machi 17, 2022.

**Hakimu:** Tangu muda huo ulishawahi kupelekwa mahakama yoyote ile?

**Alphonce:** Sijawahi, nilikuwa Oysterbay Polisi.

**Hakimu:** Uliwahi kupewa dhamana?

**Alphonce:** Hapana sikupewa dhamana.

Naye mshitakiwa wa pili, Mwenda, alidai Aprili 18, 2022 alitakiwa aende kliniki, hakupelekwa kutokana na hali hiyo macho yake yanamuuma kwa sababu alifanyiwa upasuaji wa macho, kwa hiyo anaomba apatiwe matibabu.

Pia alidai kwamba Machi 18, 2022 alikamatwa na kukaa Kituo cha Polisi Mabatini siku tatu na baadaye akahamishiwa kituo kingine na kudai kuwa alipigwa sana hadi kupata maumivu ya mguu, mkono na nyonga kwa hiyo anaomba apatiwe matibabu.

Kutokana na malalamiko hayo, Hakimu Tarimo alisema Mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za mauaji isipokuwa Mahakama Kuu ndiyo yenye mamlaka kwa hiyo, ameandika malalamiko yao kwa sababu ya kuweka kumbukumbu.

Kuhusiana na matibabu, Hakimu Tarimo aliwaeleza kwamba mahabusu zote zinatoa matibabu, kwa hiyo watatibiwa na kama hali itakuwa mbaya basi watatibiwa nje ya mahabusu na ana hakika watatibiwa.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Julai 28, mwaka huu, kwa ajili ya kutajwa. Upelelezi haujakamilika na washitakiwa wamerudishwa mahabusu kwa sababu shitaka la mauji halina dhamana.

# Auawa na tembo wakati akienda kuchota maji

**Na Allan Isack, ARUMERU**

MKAZI wa Kitongoji cha Mareu, Kijiji cha Oldonyowas Halmashauri ya Arusha, wilayani Arumeru, Sangito Pallangyo (57) ameuawa kwa kukanyagwa na tembo wakati akienda kuchota maji.

Taarifa ya kuuawa kwa mwananchi huyo, ilitolewa jana na Mwenyekiti wa Kijiji cha Oldonyowas, Geofrey Ayo, wakati Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, alipokuwa katika ziara ya kukagua ujenzi wa mabweni mawili ya wavulana katika shule ya Sekondari ya Oldonyowas.

Alisema kutokana na uhaba wa upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama wananchi wa eneo hilo, wanatembea umbali mrefu kwenda kutafuta maji hivyo wakati mwingi wakiwa njiani wanakutana na wanyama wakali.

"Mheshimiwa Naibu Waziri mwananchi huyu ameuawa wakati akiwa amekwenda kutafuta maji alitembea umbali mrefu sana, akiwa njia alikanyagwa na tembo na kupoteza maisha," alisema.

Licha ya kuzungumza hayo, aliiomba serikali kutekeleza na kukamilisha mradi wa maji safi na salama ili kutatua tatizo la wananchi wa eneo hilo kutembea umbali mrefu na kuepukana na adha ya kuuawa na wanyamapori wakali akiwamo tembo, simba na chui.

Nipashe ilimtafuta Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Justine Masejo, kupata ufafanuzi wa tukio la kuuawa kwa mwananchi huyo, alisema yuko nje ya ofisi kwa majukumu ya kikazi na aliahidi kulifuatilia na kulitolea ufafanuzi.

"Niko Karatu, bado sijapata taarifa juu ya tukio hilo lakini nitalifuatilia na nitalitolea ufafanuzi,"alisema Masejo.

# CCM yatia neno mikopo elimu ya juu

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimeelekeza serikali kuhakikisha mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu inatolewa kwa walengwa.

Ripoti ya mwaka 2020/21 ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ilibaini wanafunzi 43,053 waliokidhi vigezo walikosa mkopo ambao walihitaji Sh. bilioni 124.92 na kwa miaka mitano, wanafunzi 192,039 waliotakiwa kupata Sh. bilioni 569.5 walikosa mkopo licha ya kukidhi vigezo.

Kwa miaka mitano mfululizo, ukaguzi huo ulibaini Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB), ilitoa mikopo kwa wastani wa asilimia 72, ikimaanisha asilimia 28 ya wanafunzi waliostahili kila mwaka, walikosa mkopo, hivyo kuhatarisha uhakika wao wa kuipata elimu ya juu.

Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, aliyasema hayo jana jijini hapa ikiwa tayari HESLB imefungua dirisha la maombi ya mikopo kwa wanafunzi hao.

Akifungua kikao cha Wakuu wa Shule za Umoja wa Wazazi Tanzania, Chongolo alisema serikali imeongeza bajeti ya mikopo hiyo kwa mwaka 2022/23, ambapo Sh. Bilioni 573 zimetengwa.

"Masharti ya mikopo yamepunguzwa sana kwa lengo la kuwawezesha vijana ambao wazazi wao hawana uwezo kusoma elimu ya juu, vijana wa kitanzania kupata fursa hiyo bila kikwazo," alisema.

Chongolo alisema fedha hizo zimeongezwa kwa kiwango kikubwa ambapo kwa miaka mitatu au minne iliyopita bajeti ilikuwa Sh. bilioni 200.

"Kuna ruzuku ya Sh. bilioni tatu kwa wanafunzi watakaofanya vizuri kwenye ufaulu wa juu wa masomo ya sayansi, lengo ni kuongeza wigo na msukumo kwa vijana kusoma sayansi," alisema.

Kuhusu shule za umoja huo, Chongolo aliwapongeza wakuu hao wa shule kwa kufanikiwa kupaisha ufaulu kwa shule hizo na kuondoa alama sifuri kwenye matokeo ya kidato cha sita yaliyotangazwa hivi karibuni.

Alisema asilimia 80 hadi 90 ya wanafunzi waliofanya mtihani wa kidato cha sita mwaka huu wamepata ufaulu wa daraja la kwanza na pili huku daraja la tatu ni chache na mmoja amepata daraja la nne.

"Nawapongeza kwa kazi kubwa mliyofanya ya kufanikisha upatikanaji wa matokeo haya, nimefurahi sana sasa hivi hatupo kwenye giza, sasa hivi tunajadili mambo ya kuvutia kwenye mafanikio mliyoyajenga,"alisema.

Aliwapongeza wanafunzi wawili walioingia kumi bora kwa upande wa tahsusi za sayansi kwa wavulana ambao ni Kennedy Mcharo na Philipo Ng'eleshi wanaotoka Shule ya Sekondari Wari.

Awali, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi, Dk.Edmund Mndolwa, alisema siri ya mafanikio ni kuboreshwa kwa utawala bora kwenye shule hizo. "Hakuna shule iliyopata wanafunzi wa daraja sifuri hii ni hatua nzuri sana na inayoonesha matumaini tunakokwenda, endeleeni kuchapa kazi wakati tukisubiri mwongozo wa uendeshaji wa shule hizi ambao upo kwenye hatua za mwisho ukisubiri kupitishwa vikao vya chama,"alisema. Aliwataka kujiepusha na siasa na kuwataka kutekeleza masuala yanayohusu elimu kwenye maeneo yao ya kazi.


## TANGAZO LA MNADA

Work ethic company limited na Held auctioneer Company limited Kwa idhini tuliyopewa na **FANIKIWA MICROFINANCE COMPANY** tunapenda kuutarifu umma kuwa Tutafanya mnada wa hadhara wa Nyumba na viwanja Na magari katika maeneo tofauti katika jiji la Dar es salaam ,Wateja wanashauriwa kulipa madeni yao ndani yasiku 14 kutoka tarehe ya hili Tangazo vinginevyo Mnada utaendelea kama Tarehe za Mnada Zinavyoonekana hapa chini.

| Jina la mdaiwa | Mahali dhamana ilipo | Tarehe ya mnada |
|---|---|---|
| Amoni Eliakimu Kimaro | TOYOTA BREVIS- T709DVC | 30.07.2022 |
| James Aloyce Komba | AUDI -T214DUW | 30.07.2022 |
| Alphonce Michael Ngundana | TOYOTA RAV4-T241DUW | 30.07.2022 |
| Epafras Fidelis Jullias | Nyumba ipo Ukonga-Mongo la ndege | 30.07.2022 |
| Swaka Abbas Ally | Kiwanja kipo kigamboni | 31.07.2022 |
| Wilson Kyaruzi Ishengoma | Nyumba ipo Tabata Kimanga | 31.07.2022 |
| Emanuel Simon Mwase | Nyumba ipo Temeke | 31.07.2022 |
| Elizabeth Sylvester Malewa | Nyumba ipo majohe Mtaa wa Rada | 30.07.2022 |

**Masharti ya Mnada.**

1. Mnunuzi atakeyeshinda atalipa 25%(au Zaidi) ya bei iliyofikwa kwenye mnada na salio la (75%)litalipwa ndani ya siku kumi nne(14) kuanzia tarehe ya mnada.
2. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa mda uliotolewa atakuwa amepoteza haki zote na mali itauzwa upya.
3. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe yaTangazo.

**Kwa mawasiliano piga 0717956315(Work ethic) au 0692501004(Held auctioneer) au 0677014355(Fanikiwa**

216946902

# Jenerali Mabeyo aagwa, atoa ya moyoni

**Na Romana Mallya**

ALIYEKUWA Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Venance Mabeyo, amesema amestaafu lakini moyo wake ni Tanzania na katika kuweka msisitizo katika hilo, amelitaja neno 'Tanzania' mara nane.

Aliyasema hayo jana Dar es Salaam wakati wa sherehe za kuagwa rasmi kijeshi zilizofanyika katika Viwanja vya Abdallah Twalipo, Mgulani sherehe ambazo zilihudhuriwa na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Jacob Mkunda, na viongozi wa jeshi hilo pamoja na wastaafu.

Mbali na Mabeyo, wengine waliostaafu na kuagwa ni Meja Jenerali John Mbungo, Mnadhimu Mkuu (mstaafu), Luteni Jenerali Yacoub Mohamed, Meja Jenerali Ramadhan Mrangira, Meja Jenerali Jacob Kingu, Brigedia Jenerali Victor Kisiri, Brigedia Jenerali Fredy Kivamba na Brigedia Jenerali Athanas Mbonye.

Sherehe hizo zilipambwa na ndege za kivita ambazo zilipita kutoa heshima kwa maofisa hao wa ngazi ya juu ya jeshi pamoja na gwaride la heshima.

Akizungumza baada ya hafla hiyo, Jenerali Mabeyo alisema: "Moyo wangu ni Tanzania na ninawashauri Watanzania kuipenda Tanzania. Ukiipenda Tanzania utaitumikia Tanzania na ndiyo itapata maendeleo, vinginevyo kama huipendi Tanzania hata moyo wako wa kiutendaji utakuwa wa chini sana na dhaifu.

"Ukiipenda utataka iendelee, ninawaasa Watanzania waipende Tanzania. Nilishasema nipo jeshini miaka mingi hata ukinichanja damu yangu ni jeshi. Nimetoka jeshini lakini moyo wangu bado ni jeshi nitaendelea kuwa jeshi, bado ninalipenda jeshi nalipenda taifa langu, nitaendelea kulitumikia mpaka tone langu la mwisho," alisema.

Alipotakiwa kuzielezea wiki mbili tangu kustaafu kwake, Jenerali Mabeyo alisema amejisikia nafuu kidogo kwa sababu kila siku alikuwa anawaza anakwenda ofisini na kuna majukumu gani. Alisema kwa sasa hiyo imetoka na anafikiria aishi namna gani na wananchi.

Kuhusu matukio ya ukatili wa kijinsia na nafasi yake kama baba mwenye familia, Jenerali Mabeyo alisema kitu cha umuhimu ni malezi bora ya kifamilia na kusisitiza kuwa hilo ni lazima lianzie kwenye familia.

"Ukiwa baba, mama hata kaka ukiwa na malezi mazuri kwenye familia kwa vyovyote vile hivi vitendo vingine havitajitokeza, mara nyingi inaonekana ni kutetereka kwa malezi kuanzia ngazi ya familia, tusisitize malezi kuanzia ngazi ya familia tutapata familia zilizo bora," alisema.

Akizungumzia muda wake jeshini na uandishi wa vitabu alivyoandika alisema mara zote lazima mtu apange matumizi ya muda wakati gani afanye jukumu gani na kupumzika.

"Unapumzika unafanya nini, unapumzika labda unapata kinywaji, viburudisho hivyo, unapumzika unasema sasa ngoja niwaze jambo fulani unaliweka, unaliweka kwenye maandishi katika matumizi ya muda unakupa mwongozo.

"Sisi katika jeshi tunasema lazima uwe na matumizi ya muda hakuna wa kupoteza, ukiwa na muda wa kupoteza maana yake hufikiri chochote, lazima muda wako uupangilie.

"Nilipata muda kidogo kutunga kitabu, siyo kazi ndogo inachukua muda, unaanza na wazo, unalitengeneza, unalijenga linaimarika, unamshirikisha mwenzako analionaje wazo hilo anasema 'ninadhani linafaa' basi unaendelea mpaka mwisho," alisema.

Alipoulizwa kama ataendelea kuandika vitabu zaidi alijibu kwa kifupi kuwa, "Mwenyezi Mungu ataniongoza."

Luteni Jenerali Mstaafu Yakubu alisema amehudumu katika nafasi hiyo kuanzia 2018 hadi 2021 na kuteuliwa kuwa balozi wa Tanzania nchini Uturuki. Alisema safari yake imekuwa ndefu na yenye mafanikio makubwa mpaka kufikia kuwa Mnadhimu Mkuu wa JWTZ ambapo anajivunia katika hilo.

"Jeshi liko imara uongozi mpya umechukua madaraka, kitu cha msingi waliobaki wampe ushirikiano Mnadhimu Mkuu aliyeteuliwa na Mkuu wa Majeshi wa sasa, ili kuendeleza yale ambayo tumeyafanya na waendeleze mengine ambayo watayabuni," alisema.

Kuhusu mambo ambayo hatayasahau akiwa jeshini mpaka amestaafu, Jenerali Yakubu alisema anajivunia kuwa mtumishi wa jeshi hilo na kuna wakati akiwa Balozi wa Uturuki alipoamka na kuvaa nguo za kiraia alishtuka.

"Ninashtuka kidogo leo sare nimepeleka wapi kwa hiyo suala la sare miaka 40 si kitu cha kusahau haraka na safari imekuwa ndefu," alisema.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (wa pili kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Spika wa Bunge la Malawi, Catherine Gotani Hara (kushoto), wakati wa ziara ya Maspika wa Mabunge ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Bungeni hapo, jijini Lilongwe. Wa (pili kulia) ni Spika wa Bunge la Zambia, Nelly Mutti. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Shaka: Tutawalinda wanaotekeleza ilani

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

KATIBU Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka, amesema chama kitawalinda viongozi wake wanaotekeleza Ilani ya Uchaguzi wakiwamo wabunge, wawakilishi na madiwani ili wawatumikie wananchi.

Amesema CCM haitamvumilia wala kumfumbia macho yeyote atakajitokeza kutaka kuwavuruga kwa ajili ya kutaka kujitengenezea njia ya kuwania nafasi za uongozi katika majimbo na kata.

Shaka aliyasema hayo juzi Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba alipozungumza katika mkutano wa hadhara ulioandaliwa na Mbunge wa Gando, Salim Mussa Omari na Mwakilishi wa Gando, Mariam Thani Juma.

"Utekelezaji wa miradi unaofanywa na viongozi wa CCM unalenga kutekeleza ahadi na kutatua changamoto za wananchi katika huduma za jamii ikiwemo afya, elimu na maji. Niwahakikishie wabunge, madiwani na wawakilishi wanaotokana na CCM kwamba chama kitaendelea kuwalinda dhidi ya yeyote anayetaka kuwavuruga na kusababisha washindwe kutekeleza majukumu yao.

"Wabunge, madiwani na wawakilishi wanapaswa kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM na mwanachama yeyote mwenye malengo ya kuomba uongozi asubiri wakati mwafaka unaoruhusiwa kisheria," alisema.

Kauli hiyo ya Shaka ilitokana na kilio cha mbunge na mwakilishi wa Gando walichokitoa mbele ya mkutano huo wakilalamikia kuhusu uwepo wa baadhi ya wanachama 'wanaowashika mashati', hivyo kuchelewesha utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi pamoja na miradi ya maendeleo.

Shaka alisema kwa sasa wabunge, wawakilishi na madiwani wanapaswa kuwahudumia wananchi na kutimiza ahadi zilizonadiwa kwa wananchi.

Alisema chama kitaendelea kuwalinda na kutambua mchango wa wabunge, madiwani na wawakilishi ambao wako mstari wa mbele kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo inapokamilika inatatua changamoto katika jamii. Naye Omary alisema amedhamiria kuleta mabadiliko makubwa katika jimbo hilo ili kuondoa changamoto mbalimbali zinazowakabili wananchi.

Alisema katika kipindi cha miaka miwili tangu aingie madarakani, tayari ameshafanya mambo mbalimbali kutekeleza ilani ya uchaguzi ukiwemo ujenzi wa visima vitatu vya maji safi na salama.

Mwakilishi Juma akizungumza katika mkutano huo, aliwahakikishia wananchi kwamba yeye na mbunge wa jimbo hilo wamedhamiria kuleta mabadiliko.

Alisema katika kipindi kifupi tangu ulipomalizika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, miradi mbalimbali imetekelezwa ukiwemo ujenzi wa madarasa katika Skuli ya Mabitini na Ukunjwi.

Shaka akiwa katika ziara hiyo iliyoanza juzi visiwani humo, alipata nafasi ya kukagua miradi ya ujenzi wa madarasa na kisima cha maji safi na salama katika Jimbo la Gando, ambacho kimewapunguzia adha wananchi ya kufuata maji umbali mrefu.

# Kattanga awapa meno watendaji wa serikali

**Na Maulid Mmbaga**

KATIBU Mkuu Kiongozi, Balozi Hussein Kattanga, amewataka viongozi serikalini kuimarisha usimamizi wa rasilimali huku akiwasisitiza kutokusita kuchukua hatua za kisheria na kinidhamu dhidi ya wote watakaobainika kufanya ubadhirifu wa mali za umma.

Balozi Kattanga alitoa maagizo hayo juzi wakati akifunga kikao cha kikanuni alichofanya na Makatibu Wakuu, Makatibu Tawala wa Mikoa na Naibu Makatibu Wakuu kilichofanyika Ikulu Jijini Dar es Salaam.

Kikao hicho kilikuwa na lengo la kujadili na kubadilishana maarifa na uzoefu katika utekelezaji wa shughuli za serikali kuu, tawala za mikoa, serikali za mitaa na mashirika ya umma.

Alisema katika mkutano huo walipata fursa ya kujadili taarifa ya tathmini kuhusu mfumo wa kubuni, kupanga, kuratibu na kutekeleza shuhuli za serikali na kutoa maoni pamoja na ushauri unaolenga kuboresha mfumo huo.

"Maoni na ushauri uliotolewa utafanyiwa uchambuzi wa kina ili kuwezesha serikali kuendelea na hatua za kufanya maboresho ya mifumo yake ya ubunifu, upangaji, utekelezaji, udhibiti, ufuatiliaji na tathmini," alisema na kuongeza;

"Kupitia mkutano huu mmepata fursa ya kukumbushwa kuhusu wajibu wenu kama maofisa masuuli katika kusimamia matumizi ya rasilimali za umma, maadhimio mbalimbali yaliyofikiwa na kukubaliana katika mkutano huu hayana budi kutekelezwa na yawekewe mpango kazi wa kuyatekeleza."

Alisema ni matumaini yake kwamba wote wamehitimisha mkutano huo wakiwa na uelewa mpana zaidi kuhusu wajibu wao kama viongozi na kwamba watakwenda kutumia maarifa na uzoefu waliopata katika kuimarisha utekelezaji wa majukumu yao pamoja na kuimarisha utawala bora na uwajibikaji.

Pia alisema kutokana na umuhimu wa mkutano huo, wataendelea kupata fursa ya kuwa na mikutano ya namna hiyo kwa siku zijazo kwa lengo la kujadili masuala mengine muhimu yanayohusu utendaji wa serikali na utoaji wa huduma kwa wananchi kwa ujumla wake.

Kattanga pia alibainisha kuwa mkutano huo pia uliwawezesha kupata taarifa na uelewa zaidi kuhusu zoezi la sensa ya watu na makazi linalotarajiwa kufanyika Agosti 23, mwaka huu, na kwamba utekelezwaji wake utaiwezesha serikali kubuni, kupanga na kutekeleza mipango ya uchumi na maendeleo kwa wananchi.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Plasduce Mbossa, alisema kupitia mkutano huo wamepata uelewa kwamba kuna mambo mbalimbali yanatakiwa kurekebishwa ili kuweza kuhakikisha wanafanya biashara kwa uhuru zaidi bila kuathiri shirika.

Naye Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam, Hassan Rugwa, alisema kikao hicho kimekuwa ni muhimu kwao na lengo lake hasa lilikuwa kuongeza ufanisi na tija katika utendaji wa serikali.

# TAA yatakiwa kuboresha kiwanja cha ndege Njombe

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete, ameitaka Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA), kuanza taratibu za kutafuta fedha za kujenga uzio katika kiwanja cha ndege cha Njombe ikiwa ni sehemu ya kuanza maboresho ya kiwanja hicho.

Akizungumza juzi baada ya kutembelea kiwanja hicho, Mwakibete alisema uzalishaji wa mazao mbalimbali yakiwamo mboga na mazao ya miti, vinahitaji uwepo wa kiwanja cha kisasa kitakachokuwa kichocheo cha uchumi na kukuza biashara.

"Biashara hapa ni kubwa sana. Kiwanja hiki kikiboreshwa kitakuwa kichocheo cha ukuaji wa uchumi na kufanya biashara ziende kwa uharaka zaidi. Wafanyabiashara watakuwa na uwezo wa kuja na kufanya biashara na baadaye kuendelea na ratiba zingine," alisema.

Naibu Waziri Mwakibete aliuomba uongozi wa Mkoa wa Njombe kuzungumza na taasisi za serikali zilizo karibu na kiwanja hicho ili kuona uwezekano wa kupata eneo zaidi ambalo litatumika kwa kuongeza barabara ya kuruka na kutua ndege.

Mbunge wa Njombe Mjini, Deo Mwanyika, aliishukuru serikali kwa kuona umuhimu wa kiwanja hicho na kuanza taratibu za awali za kuboresha kiwanja hicho.

"Naipongeza sana serikali kwani nimekuwa nikizungumzia sana kiwanja hiki, kwanini wenzetu Ruvuma, Mbeya na Iringa wana viwanja vyenye lami. Ni wakati na sisi Njombe serikali ituone kwa jicho la pekee sana, hivyo tunashukuru sana kupata lami kwenye kiwanja chetu," alisema Mwanyika.

Naye Meneja wa Kiwanja hicho, Lydia Mwenisongole, alisema kwa sasa kiwanja hicho kinahudumia ndege ndogo za mashirika binafsi zenye uwezo wa kubeba abiria chini ya saba na ndege hizo huwa zinakuja mara chache kutokana na hali ya kiwanja kuwa cha nyasi.

Aliongeza kuwa kwa sasa kazi itakayofanyika ni kuzungumza na uongozi wa mkoa wakati TAA ikiendelea na taratibu za kuomba vibali husika ili kuendelea kutumika na kutoa huduma wakati serikali ikitafuta fedha.

Kiwanja cha Ndege cha Njombe ni miongoni mwa viwanja vya ndege 59 vinavyosimamiwa na TAA na kiwanja hiki kina eneo la kuruka na kutua ndege la urefu wa mita 1800 na upana wa mita 30.

# Jela miaka 40 kukutwa na meno ya tembo

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imewahukumu wakazi wawili wa Msasani Mikoroshini, Dar es Salaam, kifungo cha miaka 40 jela baada ya kupatikana na hatia ya kukutwa na vipande vitano vya meno ya tembo.

Kabla ya kuhukumiwa kifungo hicho, washtakiwa hao walikuwa wamekaa mahabusu zaidi ya miaka mitano.

Washtakiwa hao ni Abson Chaula (57) na Saidi Chekelo (42) wakati mshitakiwa wa tatu, Leornad Namie (41), aliachiwa huru baada ya upande wa mashtaka kushindwa kuthibitisha kama alikutwa na pembe mbili za nyati.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mwandamizi Ramadhani Rugemalira, baada ya kusikiliza ushahidi wa mashahidi saba wa upande wa mashitaka, utetezi wa washtakiwa pamoja na kupitia vielelezo mbalimbali vilivyotolewa mahakamani.

Rugemalira alisema katika ushahidi wote uliotolewa hakuna ushahidi unaowaunganisha mshtakiwa Chaula na Chekelo kukutwa na pembe za nyati na wala mshitakiwa Namie kukutwa na vipande vya meno ya tembo.

Alisema mahakama imemwachia huru Namie kwenye shitaka la kukutwa na pembe za nyati baada ya upande wa mashtaka kushindwa kuthibitisha kwa sababu ushahidi uliotolewa mahakamani unadai walikamata begi la kijani.

"Wamedai kuwa begi hilo lilikuwa na pembe mbili za nyati lakini begi lililotolewa mahakamani lilikuwa na rangi nyeusi. Kwa hiyo namwachia huru mshtakiwa Namie," alisema Hakimu Rugemalira.

Pia alisema mahakama imewatia hatiani Chaula na Chekelo kwa kukutwa na vipande vitano vya meno ya tembo kwa sababu mahakama haijaona kama ushahidi wa upande wa mashtaka ulijichanganya.

"Ushahidi ulieleza wazi kwamba washitakiwa walikutwa na kiroba ambacho ndani yake kulikuwa na vipande vya meno ya tembo, kwa hiyo mahakama inawatia hatiani," alisema Hakimu Rugemalira

Hakimu Rugemalira alisema kifungu walichoshitakiwa nacho washitakiwa, adhabu yake si chini ya miaka 20 jela kwa hiyo amefungwa mikono ya kufanya mabadiliko yoyote, kila mshitakiwa atatumikia miaka 20 jela.

Kabla ya adhabu hiyo kutolewa, Wakili wa Serikali Yusuph Aboud, alidai kwamba washtakiwa ni wakosaji wa mara kwanza, lakini utalii ni chanzo cha mapato kwa Serikali, kwa hiyo kuua Wanyama ni kuhatarisha sekta hiyo,wapewe adhabu kali.

Hata hivyo, washitakiwa hao waliomba Mahakama iwasamehe makosa hayo, kwa sababu ni wagonjwa na pia wanafamilia.

Inadaiwa washtakiwa hao Septemba 30, 2016 wakiwa eneo la Jangwani ndani ya wilaya ya Ilala, Dar es Salaam, walikutwa na vipande vitano vya meno ya tembo vyenye thamani ya Sh. Milioni 163.60 bila kibali cha Mkurugenzi wa Wanyamapori.

Washitakiwa hao wanadaiwa Oktoba 3, 2016 wakiwa Msasani Mikoroshini, Kinondoni walikutwa na pembe mbili za nyati zenye thamani ya Sh milioni 4.1 bila kibali.




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango (wa pili kulia), akikabidhi tuzo kwa Mkurugenzi wa Masoko na Huduma kwa wateja wa Shirika la Bima la Taifa (NIC), Yessaya Mwakifulefule, baada ya NIC kuwa mshindi wa kwanza katika sekta ya bima katika maonyesho ya 46 ya biashara ya kimataifa ya Dar es Salaam yaliyomalizika mapema wiki hii. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Bil.8/- zatengwa vita magonjwa ya mlipuko

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI imetenga Sh. bilioni nane kwa mwaka huu wa fedha zitakazotumika kuwajengea uwezo watumishi wa afya pamoja na kuwaendeleza kimasomo katika masuala ya magonjwa ya mlipuko kama vile corona.

Mganga Mkuu wa Serikali, Dk.Alfelo Sichalwe, aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati akifungua Kongamano la 10 la Sayansi lililoandaliwa na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS) lililowakutanisha wanasayansi, wataalamu wa afya na watafiti.

Dk. Sichalwe alisema hatua ya kutenga kiasi hicho ni baada ya kutokea kwa mlipuko wa ugonjwa wa corona kwa kwamba serikali imepata funzo.

Alisema: "funzo ambalo Serikali imelipata kutoka na mlipuko wa ugonjwa wa corona kwanza ni tunapaswa kuwekeza, kukusanya rasilimali pamoja na kuwekeza katika afya ya watu, miundombinu na utaalam.

"Katika kufanikisha hilo, Serikali katika mwaka wa fedha 2022/23 imetenga Sh. bilioni nane zitakazotumika kuwajengea uwezo watumishi wa afya pamoja na kuwasomesha masuala ya magonjwa wa milipuko".

Alisema pia serikali imejifunza kuwa ni vyema kutumia rasilimali zilizopo katika kujenga miundombinu, kuanzia ngazi ya chini ya afya ili ziweze kutambua wagonjwa wa corona kabla hawajapelekwa katika hospitali kubwa.

Makamu Mkuu wa MUHAS, Prof. Andrew Pembe, alisema: "Kila chuo kikuu kina malengo makuu matatu, kwanza kufundisha rasilimali watu, pili kufanya utafiti, kwamba MUHAS tunafanya utafiti unaohusu afya ya binadamu."

Alisema kazi ya tatu ya chuo kikuu ni kutoa ushauri wa kitaalamu, kwamba MUHAS wamekuwa wakitoa ushauri katika masuala ya afya ya mimea. Alisema MUHAS imejikita katika kufanya utafiti ambao nchi imeweka kipaumbele.

Prof. Pembe alisema wakati wa mlipuko wa ugonjwa wa corona, MUHAS walifanya utafiti wa aina mbalimbali ikiwamo utambuzi wa mgonjwa wa corona, kuwasaidia wagonjwa wa corona, kutokana na mabadiliko ya ugonjwa wa corona pamoja na mabadiliko ya Watanzania kujikinga na ugonjwa corona.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga imarisheni timu B kuokoa mamilioni

**MSIMU** mpya wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara inayoshirikisha timu 16 kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini unatarajiwa kufunguliwa rasmi ifikapo Agosti 17, mwaka huu.

Lakini ligi hiyo itafunguliwa na mchezo wa Ngao ya Jamii utakaochezwa Agosti 13, mwaka huu kwa kuwakutanisha mabingwa wapya Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga dhidi ya mshindi wa pili, Simba.

Watani hao wa jadi kutoka Kariakoo jijini Dar es Salaam wanakutana kwa sababu Yanga ndio bingwa pia wa mashindano ya Kombe la FA, kama ilivyokuwa kwa msimu uliopita ambapo Wekundu wa Msimbazi alibeba makombe yote.

Lakini kuelekea msimu mpya, Simba, Yanga na timu nyingine zote zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara ziko katika mchakato wa kusajili wachezaji wapya ili kuimarisha na kuboresha vikosi vyao kwa ajili ya msimu huo wa 2022/2023.

Timu zote zinasema zinafanya usajili kwa kuzingatia mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti maalumu zilizowasilishwa na makocha wao baada ya kubaini mapungufu mbalimbali katika msimu uliomalizika.

Mchakato wa usajili huwa unafanywa na timu zote, kuanzia bingwa hadi timu mpya zilizopanda daraja, timu zilizoshuka daraja pia hujiimarisha kwa ajili ya kwenda kupambana katika changamoto mpya waliyoangukia.

Lakini pia timu zilizomaliza nje ya malengo yake pia hufanya jitihada mbalimbali za kujenga vikosi vyao kwa ajili ya kuanza msimu mpya wakiwa imara. Unaweza kusema jambo hili ni la kawaida, lakini kwa upande wa Ligi Kuu Tanzania Bara hali imebadilika kutokana na motisha inayotolewa na wadhamini wenza wa ligi hiyo ambao wana haki ya kuonyesha michezo yote kwenye televisheni ambao ni Kampuni ya Azam Media.

Wadhamini hawa hutoa motisha kuanzia kwa bingwa mpaka timu iliyoshuka daraja lakini kwa viwango vya fedha tofauti. Kwa maana hiyo, msimu uliopita kila timu ilijiwekea malengo ili kupata motisha kubwa ambao inaamini itawasaidia kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya.

Ili kupata vikosi imara, kila timu imekuwa ikihangaika ndani na nje ya Tanzania kusajili wachezaji watakaowasaidia, lakini wakati ikifanya hivi kuimarisha vikosi vyao vya kwanza, timu zimekuwa nyuma kusajili wachezaji wenye vipaji kwa ajili ya timu zao za vijana za umri chini ya miaka 17 na 20, ambazo kwa hakika ndio msingi wa kupata timu A.

Mbali na kufanya mchujo (scouting) ya kupata nyota wanaosajiliwa kwa ajili ya timu hizo, kumekuwa na tatizo la kushindwa kuwatunza yosso hao kama inavyotakiwa na matokeo yake wanaposhiriki katika mashindano ya U-17 na u-20, hutolewa mapema au baadhi ya timu hushindwa kupeleka yosso hao kuchuana.

Umefika wakati, Simba, Yanga, Azam FC kuwekeza kikamilifu katika timu za vijana kwa sababu kwa kufanya hivyo, sio tu kutawapa nafasi yosso wao kuonekana, lakini itawapunguzia gharama ya kutumia kiasi kikubwa cha fedha kusajili wachezaji wa kigeni au kutoka katika timu nyingine.


Klabu inapokuwa na timu imara za vijana, basi hupata nafasi ya kupandisha baadhi ya nyota wake walioiva na hivyo, hupunguza bajeti ya kusajili wachezaji wapya kutoka sehemu nyingine.

Ukiondoa vigogo hawa wa soka wenye wadhamini mbalimbali pamoja na Azam FC inayomilikiwa na mfanyabiashara mkubwa wa hapa nchini, timu nyingine zinatakiwa kujikita kutunza timu za vijana ili ziwasaidie katika kuboresha vikosi vyao bila ya kutumia fedha kiasi kikubwa kama ilivyo sasa.

Kwa kufanya hivi, si tu kutaokoa mamilioni ya fedha kusajili wachezaji wageni au kutoka nje ya klabu husika, lakini pia kutasaidia kuzijenga timu za taifa ambazo zinategemea kupata wachezaji kutoka kwa klabu za hapa nchini. Ushauri huu pia unawahusu wote wanaomiliki timu zinazoshiriki Ligi Kuu ya Soka ya Wanawake Tanzania ingawa inafahamika inahitaji kuwa na bajeti ya kutosha kuhudumia timu B.

Kama ambavyo Simba, Yanga, Azam na timu nyingine zina ndoto ya kufikia mafanikio ambayo Al Ahly, Zamalek kutoka Misri, Mamelodi Sundowns ( Afrika Kusini) au RS Berkane ya Morocco, basi wakati umefika wakafuata nyao zao kwa kuwa na akademi au timu za vijana imara na si kukusanya na kuwaweka yosso pamoja kutimiza matakwa yaliyotolewa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) ili kushiriki Ligi Kuu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Simba SC, Yanga usajili wa gharama, halafu zinabebwa

Na Adam Fungamwango

**HABARI** kubwa kwa sasa nchini Tanzania ni usajili wa wachezaji kwa ajili ya msimu ujao wa mashindano.

Klabu zilizotia fora kwa usajili mpaka sasa ni tatu, ambazo ni Simba, Yanga na Azam FC, zote za jijini Dar es Salaam.

Kila klabu imeshusha vifaa, wachezaji wa kimataifa ambao inaamini watakuwa chachu kuelekea msimu ujao kwani zote zitaiwakilisha Tanzania katika michuano ya kimataifa. Simba na Yanga zitacheza Ligi ya Mabingwa Afrika wakati Azam itaenda kuchuana katika mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Azam imewasajili wachezaji raia wa Ivory Coast, Tape Edinho, Kipre Junior, Mnigeria Issa Ndala, kipa Ali Ahmada ambaye ni raia wa Comoro na Mghana James Akamanko.

Lakini kama ilivyo kwa soka la Tanzania, macho ya mashabiki yapo kwa klabu za Simba na Yanga.

Kwa upande wa Simba, yenyewe inaendelea kusajili, na tayari imeshaanza kutangaza baadhi ya wachezaji iliyowatia mikononi.

Usajili wao uliotikisa mpaka sasa ni wa mchezaji wa kimataifa wa Ghana, Augutine Okrah.

Ni usajili uliotikisa nchini pamoja na kwao Ghana, wakifuatilia mchezaji huyo ambaye kwa maoni ya wengi alifaa kwenda kucheza soka la kulipwa barani Ulaya.

Ndiyo mchezaji pekee kama si wawili wanaoitwa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa wakicheza soka la kulipwa Afrika.

Wakati Simba wakifanya hivyo, Yanga nayo ikashusha kifaa kutoka Burkina Faso ambacho kilikuwa kinacheza soka la kulipwa nchini Ivory Coast kwenye klabu ya Asec Mimosas. Anaitwa Stephane Aziz Ki.

Nao umekuwa ni usajili wa kushtusha kwa mashabiki wa soka, hasa barani Afrika ambao sasa wameanza kuiangalia Tanzania na usajili wake kwa wachezaji wa Afrika Magharibi.

Vita au mbwembwe za usajili hapa Tanzania hazikuanza leo. Ni za enzi na enzi. Tofauti yake zamani zilikuwa zikisajili wachezaji wenye umri mkubwa au wenye viwango duni kutoka Afrika Magharibi, lakini wachezaji wa kawaida walikuwa wakisajiliwa kutoka Rwanda, Burundi, Kenya na Uganda.

Baadaye tukaanza kuona Simba na Yanga zikibadilika na kuanza kusajili wachezaji wenye viwango vikubwa kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Zambia.

Kwa sasa tunaanza kuona zimeanza kusajili wachezaji wa viwango vya juu kutoka Afrika Magharibi.

Haya ni maendeleo makubwa katika soka la nchi hii kwa sababu Ligi Kuu Tanzania Bara itaanza kufuatiliwa mpaka kwenye nchi hizo, baada ya mashabiki wa Kenya, Rwanda, Burundi, Zambia wakifanya hivyo kwa ajili ya kuona wachezaji wao.

Lakini bado binafsi natatizwa na kitu kimoja. Nacho ni waamuzi wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Pamoja na timu hizi zinasajili wachezaji wa viwango vya juu na kuziacha klabu zingine zikipambana kunyang'anyana wachezaji wa Kibongo wenye viwango vya kawaida, lakini baadhi yao maamuzi yao yanakuwa ya kuzibeba hizo hizo timu zenye wachezaji wenye uwezo.

Huu ni unyanyasaji na ukatishaji tamaa kwa wachezaji hasa wa Kitanzania. Kwanza hawaimbwi kama hawa wa nje. Sawa ni kwa sababu ya viwango vyao. Lakini hata pale wanapopambana kutaka kuonyesha uhodari wao na kuionyesha Afrika na dunia kama wanaweza, lakini unakuta waamuzi wanawafanya waonekane hawajui.

Timu ya Ligi Kuu inaweza kucheza kimkakati na mfumo mzuri huku wachezaji wake Wazawa wakijitolea kwa asilimia 100 kupambana na Simba au Yanga zenye nyota wa kigeni, lakini kwa makusudi au bahati mbaya wamekuwa wakiwatoa kwenye mchezo kwa kuzibeba timu kubwa.

Kutokana na gharama ambazo Simba na Yanga inatumia kwenye usajili, ifike wakati waamuzi waache viwango vifanye kazi uwanjani na si kuwaongezea wachezaji wa kigeni viwango na kuwashusha kwa makusudi Watanzania waonekane hawajui.

Kama timu ina wachezaji bora iachwe ishinde kwa uwezo wake. Ni dhambi na aibu kubwa kuidhulumu timu yenye wachezaji wenye viwango vya kawaida ambao wamepambana na kutoa jasho kuwadhibiti wale wa viwango vikubwa, lakini mwamuzi analazimisha waonekane hawajui chochote kwa kuzibeba tu timu kubwa.

# Mbunge akemea siasa majitaka

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MBUNGE wa Shinyanga Mjini, Patrobasi Katambi, amekemea Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Wilaya ya Shinyanga Mjini na kutaka kuacha kufanya siasa za kufitinisha viongozi.

Alibainisha hayo juzi kwenye kikao cha UVCCM Wilaya ya Shinyanga, kilichofanyika ukumbi wa mikutano wa CCM wilayani hapa.

Katambi ambaye pia ni Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, alisema vijana wa CCM hawapaswi kujiingiza kwenye siasa za kufitinisha viongozi, bali wanatakiwa kuwa wasuluhishi na kuleta maendeleo ndani ya chama na kudumisha amani na siyo kuchochea vurugu.

"Nawaombeni vijana wenzangu msikubali kushawishiwa na mtu wala kuyumbishwa na kukubali kufitinisha watu, hii ni kwa ajili ya maslahi ya chama na chama chetu kinasema fitina kwetu mwiko, hivyo hamtakiwi kukivuruga chama, bali tukijenge tusiwe na roho mbaya tuwe na upendo wa kweli," alisema Katambi.

"Mimi mwenyewe sitakubali kuyumbishwa na mtu yeyote, huwa ninasimamia haki hasa pale linapokuja suala la maslahi ya chama, na tunahitaji sisi vijana tumtetee na kumpigania Mwenyekiti wetu wa CCM Taifa Rais Samia Suluhu Hassan na siyo kukalia kufitinisha watu," aliongeza.

Naye Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Shinyanga Mjini, Ally Majeshi, aliwataka vijana wasikubali kuwa vibaraka wa watu, na kuacha pia kukaa kwenye magenge na kulishana maneno yasiyofaa ambayo hutengeneza majungu na kuvuruga amani ya chama.

"Kijana wa CCM hana sifa ya kukaa kwenye magenge na kulishwa maneno na kumtengenezea kashifa kiongozi ama mtu yeyote, mjiepushe kuwa vibaraka wa watu wala kundi la mtu, tukimgundua kijana wa namna hiyo tunamuondoa", alisema Majeshi.

Aidha, Mwenyekiti wa UVCCM Wilaya ya Shinyanga Mjini, Dotto Joshua, aliwasisitiza vijana waendelee kufanya kazi kwa bidii na kwa ushirikiano, ili kuhakikisha shughuli za chama zinasonga mbele.

Kwa upande wake Katibu wa UVCCM wilaya ya Shinyanga Mjini Naibu Katalambula, akisoma taarifa ya umoja huo wa vijana, alisema wamejipanga vizuri katika kufanya kazi mbalimbali za chama, pamoja na kusimamia vizuri zoezi zima la uchaguzi ndani ya chama hicho ambalo linafanyika mwaka huu.

# Mkenda acharuka ubora wa elimu

**Na Mwandishi Wetu,** IRINGA

SERIKALI imesema kuwa haitafanya uzembe kwenye usimamizi wa ubora wa elimu, hivyo imeitaka Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) kuendeleza udhibiti wa ubora wa elimu katika ngazi ya vyuo vikuu.

TCU imekumbushwa lengo la kuanzishwa kwake ikiwa ni pamoja kuhakikisha inasimamia kwa weledi mkubwa elimu ya vyuo vikuu nchini kwa kufanya utambuzi na uidhinishaji wa elimu ya vyuo vikuu kabla ya chuo kikuu chochote kuanza.

Akizungumza juzi wakati wa sherehe za siku ya Chuo Kikuu cha Iringa, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof Adolf Mkenda, alisema hakutakuwa na shinikizo lolote la utoaji wa digrii zisizokidhi vigezo kwenye kazi za kitaaluma, hivyo serikali itahakikisha kuwa ubora wa elimu unasimamiwa ipasavyo.

Waziri Mkenda alisema kuwa ili kuwe na wataalamu wazuri katika sekta ya afya, ni vyema kama kuna uwezekano vigezo viongezwe hususani katika usimamizi wa masuala ya tiba ili kuakisi ubora wa elimu nchini. "Tukicheza na ubora wa elimu tutaua nchi yetu na hapa nchini vipo baadhi ya vyuo binafsi ambavyo ili viwe na wanafunzi wengi vinatoa GPA kubwa pasina kujali ubora na uwezo wa wahitimu wao," alisema na kuongeza kuwa:

"Tanzania si kapu la kutuletea digrii feki, hivyo ubora wa elimu utasimamiwa bila woga na presha ya watu wenye fedha au wanasiasa, lakini na nyie TCU mtoe majibu kwa wakati mkichelewa hatutaelewana."

Prof. Mkenda alisema vigezo vya udahili na utoaji elimu vinafahamika, ubora unafahamika, hivyo tathmini ikifanyika vikaangaliwa vigezo kila mtu atapata kwa mujibu wa vigezo hivyo na si vinginevyo.

"Nchi yetu haiwezi kuendelea kwa kupeana nafasi kwa undungu na kwa upendeleo ila tunaweza tukaendelea tukipeana nafasi kwa uwezo, vipaji na juhudi si kwa sababu baba yako ana hela nyingi ndiyo upewe hiyo," alisisitiza.

Waziri Mkenda alisema mtu unaweza kuwa na akili nyingi lakini mvivu na mlevi na una uwezo mkubwa lakini mzembe, hivyo lazima TCU isimamie ubora na kufanya kazi kwa kasi zaidi ili elimu ya Tanzania isiwe ni bora elimu bali elimu bora.



Mafundi wakisawazisha na kushindilia udongo katika bustani inayotenganisha barabara mpya ya kuelekea stendi kuu ya Magufuli Mbezi Luis, Manispaa ya Ubungo Dar es Salaam jana, ambayo imepanuliwa na kuwa na sehemu mbili, ili kupunguza msongamano wa mabasi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Bil. 18.2/- kumaliza kero barabara, madaraja

**Na Mary Geofrey**

SERIKALI imetenga Sh. bilioni 18.2 kwa ajili ya miradi ya ujenzi wa barabara na madaraja mkoani Mbeya.

Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA), Mhandisi Florian Kabaka, alibainisha hayo jana wakati wa ukaguzi wa daraja la Mwasanga linalounganisha kata za Mwakibete na Tembela, Halmashauri ya Jiji la Mbeya.

"Tunamshukuru sana Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuridhia kutoa kiasi cha fedha hizo Sh. bilioni 18.2 zinazoenda kuwanufaisha wananchi wa mkoa wa Mbeya," alisema Kabaka.

Alisema miradi hiyo itahusisha ujenzi wa daraja la Mwasanga litakalogharimu Sh. bilioni 1.9 na pia fedha hizo zitajenga kwa kiwango cha lami barabara za Inyala-Simambwe (Km 16.7) Sh. bilioni 7.05; Lupeta-Izumbwe (Km 10) Sh. bilioni 4.5 Masebe-Lutete (Km 7.2) Sh. bilioni 2.5 na Masebe-Bugoba kibaoni (Km 5) Sh. 2.1.

"Wananchi wafahamu wazi kuwa fedha hizi ziko tayari zimeshakasimiwa na si za kutafuta. Sasa ni kazi ya makandarasi kuongeza kasi ya ujenzi ili miradi ikamilike kwa wakati na kuleta manufaa kwa wananchi," alisema Kabaka.

Pia aliagiza watendaji kuongeza usimamizi na kulipa makandarasi kwa wakati ili kusiwe na kisingizio chochote kwa kuwa fedha zipo.

Naye mkazi wa Mwakibete, Maonyeshwe Mbwiga, aliishukuru serikali kwa kuwajengea daraja litakalo waondolea kero walizokuwa wakipata.

"Hili daraja mwaka juzi lilibomolewa na mvua na kuna watu wawili walipoteza maisha, mbunge wetu, Dk. Tulia, Ackson alikuja hapa na kuahidi kuwa daraja jipya litajengwa. Sasa tunaona kweli mafundi wapo wanaendelea na ujenzi. Hata sisi wananchi tunaona kweli serikali inafanya kazi, tunashukuru sana," alisema Mbwiga.

Naye Aron Nyembele, mwanafunzi wa Sekondari Mwakibete alisema kuwa walikuwa wanapata shida kuvuka baada ya daraja kubomoka na wamefurahi kuona daraja jipya na la kisasa linajengwa.

" Tunashukuru kuona daraja hili linajengwa sasa tutapita kwa amani bila wasiwasi wowote. Tunamshukuru sana Rais wetu Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kutujali,"alisema Nyembele.

Bodi ya Ushauri TARURA inaendelea na ziara ya kikazi mkoani Mbeya kukagua miradi mbalimbali inayoendelea kutekelezwa na iliyo kamilika ili kuhakikisha adhma ya serikali ya kuboresha na kufungua barabara mpya za Vijijini na Mijini na kuwaletea maendeleo wananchi inatimia.

# Korti yatoa msimamo dhamana vigogo TPA

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imesema haiwezi kuendelea na hatua ya dhamana katika kesi ya uhujumu uchumi inayowakabili vigogo watano Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) kwa sababu bado haijaliona jalada la Mahakama Kuu lenye masharti ya dhamana.

Vigogo hao ni aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu, Madeni Kipande, Peter Gawile (58) Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Utawala, Casmily Lujegi (65) Mwenyekiti wa Bodi ya Ununuzi, Mashaka Kisanta (59) Mkurugenzi wa Ununuzi na Kilian Chale (51) Kaimu Mkurugenzi wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

Mahakama hiyo ilifikia uamuzi huo baada ya Wakili wa Gawile na Kisanta, Deogratius Mwarabu, kudai juzi mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Ramadhani Rugemalira, kuwa wameshamaliza taratibu zote za dhamana Mahakama Kuu na pia jalada limeshafikishwa mahakamani.

Alidai kwamba wameshafanya taratibu zote, hivyo wanachosubiri ni jalada lenye masharti ya dhamana kufikishwa Kisutu kutoka Mahakama Kuu kwa sababu kutokana na kiasi cha fedha wanachoshitakiwa nacho, dhamana inaombwa huko.

"Kwa mujibu wetu jalada limeshaletwa hapa Kisutu, kwa hiyo hakimu mhusika ndiyo atawaelekeza mambo ya dhamana yanavyotakiwa,"alidai Mwarabu

Baada ya Mwarabu kudai hayo, Hakimu Rugemalira alisema hawezi kuendelea na hatua yoyote kwa sababu bado hajaliona jalada kutoka Mahakama Kuu ambalo linaonyesha kwamba wamemaliza taratibu zote za dhamana.

Hakimu Rugemalira aliahirisha kesi hiyo hadi Julai 26,2022 kwa kutajwa.

Awali, Wakili wa Serikali, Timotheo Mmari, alidai kwamba kesi hiyo ililetwa kwa kutajwa na upelelezi bado haujakamilika.

Wakati washtakiwa wakifikishwa mahakamani, Kipande bado amelazwa katika Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI) kutokana na upasuaji aliofanyiwa.

Washitawa hao wanakabiliwa na mashitaka ya kuisababishia mamlaka hiyo hasara ya Dola za Marekani milioni 1.8 sawa na Sh bilioni 4.2.

# Wanaotaka kusoma nje kudahiliwa papo kwa papo

**Na Joseph Mwendapole**

VYUO vikuu 10 vya nje vimethibitisha kushiriki Maonyesho ya 17 ya Vyuo Vikuu yanayotarajiwa kuanza Jumatatu huku wanafunzi wanaotaka kusoma nje ya nchi watapata udahili wa papo kwa papo.

Miongoni mwa vyuo vikuu hivyo vinavyoshiriki kwa mwavuli wa Wakala wa Elimu Nje ya Nchi, Global Education Link (GEL) ni MM, Sharda, CT, Geomedi, GELISM, Lovely Professional University.

Vyuo vingine vya nje vitakavyoshiriki maonyesho hayo yanayofanyika kila mwaka katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam ni vya kutoka India, Iran Cyprus, Uturuki, Georgia, Canada, Australia, Urusi, Marekani na Uingereza.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkurugenzi Mtendaji wa wa GEL, Abdulmalick Mollel, alisema maonyesho hayo yameandaliwa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) yanatarajiwa kuanza keshokutwa na kumalizika Jumamosi.

Alisema hayo ni maonyesho makubwa yanayoandaliwa na TCU ambayo yatakutanisha vyuo vikuu vingi na taasisi mbalimbali za elimu.

"Global Education Link ambao ni mawakala wakubwa wa elimu nje ya nchi, tutashiriki tena tuna shiriki kikamilifu na lengo ni kuhakikisha wanafunzi waliomaliza kidato cha sita na wangependa kwenda nje ya nchi tutawadahili papo kwa papo kupitia maonyesho hayo," alisema. Mollel alisema GEL itatoa taarifa mbalimbali zitakazowapa uelewa wanafunzi kuhusu ubora wa vyuo, aina ya kozi zilizopo kwenye vyuo hivyo na mazingira ya vyuo hivyo ili wafanye chaguo sahihi.

"Hizi ni taarifa ambazo kwenye maonyesho haya tutazitoa kwa kila nchi ambayo mwanafunzi anataka kwenda kusoma kwa gharama zake, utaratibu wa Visa na kama kuna mitihani inapaswa kufanyika na utaratibu wa lini wanafunzi wataweza kujiunga na vyuo vikuu," alisema Mollel. Alisema kwenye maonyesho hayo, GEL itawakutanisha wanafunzi Watanzania wanaotaka kusoma astashahada, shahada ya kwanza, shahada ya umahiri na ile ya Uzamivu (PhD) na vyuo vikuu moja kwa moja ambavyo vitakuwa kwenye mabanda ya GEL ili kuwapatia fursa kwenda nje.

Kama kutakuwa na vyuo vikuu vya ndani vitakavyoshiriki kwenye maonyesho hayo, alisema vitapata fursa ya kusaini mikataba ya ushirikiano na vyuo vya nje kwa ajili ya kubadilishana wanafunzi wa Tanzania kwenda nje ya nchi na wale wa nje kuja Tanzania.

"Kuna wanafunzi huwa wanakwama wanapotaka kwenda nje kama Uingereza kwani huwa wanatakiwa kufanya mitihani na wengi unakuta hawana uelewa wa mitihani hii inayoratibiwa na British Council sasa kwenye maonyesho haya Bitish Council watashiriki kwenye banda la GEL kuwaelekeza namna ya kufanya ili waende kusoma huko," alisema.

" Vyuo vya India, Iran Cyprus, Uturuki, Georgia, Canada na Australia vitakuwepo kwa hiyo katika maonyesho haya Global Education Link inaona ilete dunia kupitia mabara tofauti hapa Tanzania na wanafunzi wanaotaka kozi za udaktari wasihofu zipo na kuna ufamasia, meno, mamacheza, maabara" alisema Mollel



Mwanafunzi wa mwaka wa pili katika Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki (HKMU), Jenise Mpanju (kulia), akimpima shinikizo la damu mmoja wa wananchi waliofika kwenye kambi ya mwezi mmoja ya kupima afya bure ikiwemo magonjwa afya ya akili, inayoendelea Mlimani City, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Idadi ya watalii yazidi kuongezeka

**Na Romana Mallya**

IDADI ya watalii katika kipindi Januari hadi Mei, mwaka huu, imeongezeka na kufikia 458,048 ikilinganishwa na 317,270 walioingia kipindi kama hicho mwaka jana huku Ufaransa ikiongoza kuleta wengi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Kaimu Mkurugenzi za Takwimu za Uchumi wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Daniel Masolwa, alisema idadi hiyo ni ongezeko watalii 140,778 sawa na asilimia 44.4.

Masolwa alisema kati ya watalii 458,048 walioingia nchini mwaka huu, 137,758 wameingia kupitia Zanzibar ambao ni sawa na asilimia 30.1.

"Watalii walioingia nchini Mei pekee waliongezeka hadi 89,271 ikilinganishwa na watalii 42,173 walioingia Mei 2021, sawa na ongezeko la asilimia 117.7. Idadi hii ya watalii walioongezeka mwezi Mei, mwaka huu ilikuwa zaidi ya mara mbili ya wale walioingia katika kipindi kama hicho mwaka jana.

Alisema hiyo inatokana na kazi iliyofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan kupitia filamu ya The Royal Tour iliyozindulia Aprili 25, mwaka huu.

Pia alisema takwimu hizo zimeonyesha namna filamu hiyo ilivyofanikiwa kuongeza idadi ya watalii wanaoitembelea Tanzania. Masolwa alisema Januari, mwaka jana, idadi ya watalii ilikuwa ni 79,116 na mwaka huu wamefikia 94,441 ikiwa ni ongezeko la watalii 15,325 sawa na asilimia 19.4.

"Februari mwaka jana walikuwa 79,730 na mwaka 2022 wameongezeka na kufikia 101,042 ikiwa ni ongezeko la watalii 21,312 sawa na asilimia 26.7. Machi mwaka jana walikuwa 72,285 na mwaka huu wamefikia 93,889 ikiwa ni ongezeko la watalii 21,604 sawa na asilimia 29.9. "Aprili mwaka jana 43,966 na mwaka huu wameongezeka na kufikia 79,405 ikiwa ni ongezeko la watalii 35,439 sawa na asilimia 80.6. Mwezi Mei mwaka jana watalii walikuwa ni 42,173 na mwaka huu wamefikia 89,271 ikiwa ni ongezeko la watalii 47,098 sawa na asilimia 111.7." Masolya alisema watalii walioingia nchini kutoka nchi zilizo nje ya Bara la Afrika kwa mchanganuo wa utaifa katika kipindi cha Januari hadi Mei, mwaka huu, unaonyesha kuwa Ufaransa iliongoza kwa idadi kubwa zaidi ambao ni 28,115 ikifuatiwa na Poland waliokuja 22,651.

Alisema nchi zingine na idadi kwenye mabano ni Marekani watalii (21,661), Ujerumani (16,527), Uingereza (14,136) na India (13,641).

Alisema idadi kubwa ya watalii walioingia nchini kutoka nje ya Bara la Afrika kwa mwezi Mei mwaka huu pekee, waliotoka Marekani (5,606), Ufaransa (4,456) India (4,211), Uingereza 3,294) na Ujerumani (3,160).



## HABARI DODOMA

### Korea Kusini kuineemesha Dodoma sekta afya

**Na Mwandishi Wetu,** KONGWA

SHIRIKA la Serikali ya Korea Kusini linalojishughulisha na masuala ya huduma za afya kimataifa (KOFIH), limetoa Sh. milioni 850 kwa ajili ya uboreshaji huduma za afya katika wilaya za Kongwa na Mpwapwa, mkoani Dodoma.

Rais wa KOFIH, Prof. Chang-yup Kim, aliyabainisha hayo jana alipotembelea kujionea utoaji wa huduma za afya kwenye Hospitali ya Wilaya ya Kongwa.

KOFIH kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Mkoa wa Dodoma inatekeleza Mradi wa Uboreshaji wa Huduma za Afya ya Uzazi na Mtoto katika halmashauri za Kongwa na Mpwapwa.

Prof.Kim alisema ili kutekeleza azma hiyo shirika hilo limetoa fedha kwa ajili ya kusaidia hospitali hiyo katika ununuzi wa vifaa tiba vikiwapo mashine mbili za usingizi, vifaa vya maabara na vifaa vya kujikinga na maambukizi.

"Kiasi cha fedha ambazo KOFIH imetoa kwa ajili ya Hospitali ya Kongwa ni Sh. Milioni 186. Pia imetoa Sh. milioni 460 kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya vituo vya Afya vya Chamkoroma (Kongwa) na Rudi (Mpwapwa),"alisema.

Pia alisema KOFIN imetoa Sh. milioni 204 kwa ajili ya ununuzi wa mashine ya mionzi ya Hospitali ya Wilaya ya Mpwapwa.

"Mradi KOFIH nchini Tanzania ni wa miaka mitano 2021/2026 ambao unahusisha uboreshaji wa miundombinu katika vituo vya kutolea huduma za afya ili kuwezesha utoaji wa Huduma za dharura za upasuaji, ununuzi na uwekaji wa vifaa tiba kwa ajili ya kuwezesha utoaji wa huduma bora za afya," alisema.

Kadhalika, alisema shirika hilo pia linatoa mafunzo mbalimbali kwa watumishi wa afya ili kuwajengea uwezo wa kutoa huduma bora.

# Simbachawene ataka mageuzi katika kilimo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, George Simbachawene, amewataka watendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa kufanya mageuzi makubwa ya kilimo kwa kuwekeza katika miradi ya kimkakati itakayoongeza uzalishaji. Simbachawene ambaye pia ni Mbunge wa Kibakwe, aliyasema hayo juzi katika ziara jimboni mwake iliyolenga kuzungumza na wananchi na kupokea kero zao.

Alisema serikali katika bajeti yake ya mwaka 2022/23 imeongeza bajeti ya kilimo kutoka Sh. bilioni 200 mpaka Sh.bilioni 900.

"Fedha hizi ni nyingi zitapelekwa vijijini katika ujenzi wa miradi ya kimkakati ya kilimo, hivyo ni vyema wananchi wakachangamkia fursa hiyo, lakini watendaji na madiwani wa Mpwapwa mhakikishe mageuzi haya makubwa ya kilimo yanaonekana kwa wananchi,"alisema.

Katika hatua nyingine, Simbachawene alipongeza wilaya hiyo kwa utekelezaji mzuri wa uwekaji wa anuani za makazi.

"Nimefurahi kwa halmashauri kutekeleza vyema uwekaji wa anuani za makazi, nimeona mpaka nyumba za nyasi zimewekewa namba na mitaa ina majina. Ni kazi nzuri nadhani wengine wanapaswa kuja kujifunza hapa," alisema.

Kuhusu miundombinu ya barabara, Simbachawene alisema halmashauri hiyo imetenga Sh. milioni 626 kwa ajili ya kukarabati barabara ya Makose-Idodoma.

Simbachawene alihimiza wananchi kushiriki katika kutunza barabara na kuwa na utaratibu wa kurejesha barabara pale wanapoona imebomoka.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mpwapwa ambaye pia ni Diwani wa Mpwapwa Mjini, George Fuime, alisema halmashauri ina mpango wa kukarabati majengo yote chakavu ya shule za msingi ili kujenga mazingira bora ya kujifunza.

Aliwataka wananchi kuacha kufyeka na kukata miti katika milima ili kulinda vyanzo vya maji.




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango (kulia) akiwa katika picha ya pamoja na washindi wa tuzo mbalimbali baada ya kufunga maonyesho ya 46 ya biashara ya kimataifa ya Dar es Salaam ambapo kampuni ya Geita Gold Mine Ltd (GGML), iliibuka mshindi wa tuzo ya mwajiri bora anayezingatia taratibu za Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) na msafirishaji bora wa madini nje ya nchi na kupokewa na Mwanasheria Mwandamizi wa GGML, David Nzaligo (kushoto). Katikati ni Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wizara yaanza kupima afya udongo kubaini mbolea kutumika shambani

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WIZARA ya Kilimo imeanza kupima afya ya udongo nchi nzima ili kuwasaidia wakulima kutambua mazao gani walime na aina ipi ya mbolea watumie ili kilimo chao kiwe na tija.

Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, alibainisha hayo jana alipokuwa akizungumza na wakulima wa kata ya Hombolo, jijini Dodoma baada ya kutembelea na kukagua mashamba darasa yaliyotumia mbolea zinazozalishwa na kiwanda kipya cha Mbolea cha Itracom.

"Kazi hii ya upimaji udongo itatusaidia pia kuwa na kanda za kilimo ili mazao yalimwe kwa kanda siyo kila mkulima kujipandia mazao ambayo yeye anaona yanamfurahisha ili kusadia pia wakulima kuacha kulima kilimo cha kubahatisha," alisema Mavunde.

Pia aliwataka wakulima wote nchini kuzingatia matumizi ya mbolea katika kilimo chao ili kiwe na tija tofauti na ilivyo sasa ambapo wanawekeza nguvu nyingi lakini tija ni kidogo sana.

"Matumizi ya mbolea katika kilimo hivi sasa hayakwepeki kama mkulima anataka kupata tija tuachane kabisa na dhana ya kuwa kutumia mbolea unaharibu ardhi," alisema Mavunde.

Kadhalika, alisema kupitia kilimo nchi itakuwa na uhakika wa chakula, ajira, kukuza uchumi wa mtu mmojammoja na taifa kwa ujumla.

"Katika bajeti ya mwaka huu kwenye kilimo, kila sekta imeongezewa kiasi kikubwa cha fedha ikiwemo katika utafiti na umwagiliaji. Niwaombe watafiti mnapofanya utafiti wenu hakikisheni matokeo yanawafikia wakulima mapema ili wapate mbinu bora za kilimo na kuongeza tija," alisema.

Pia alisema serikali inapanga kufufua mabonde yote ambayo yanafaa kwa kilimo cha umwagiliaji ili kusaidia wakulima kulima kwa kipindi chote cha mwaka.

"Lazima tuwekeze katika sekta hii ya kilimo cha umwagiliaji ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi ili mvua zinapo kuwa chache kama mwaka huu tunakua na uhakika wa chakula kwa kutumia umwagiliaji," alisisitiza Mavunde.

Naye, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dk. Stefan Ngaito, aliwatoa hofu wakulima kuhusu matumizi ya mbolea.

Alisema wamekuwa wakipima na kuthibitisha ubora wa mbolea zote za ndani na nje ya nchi.

"Niwasihi wakulima nchini kuhakikisha kuwa wanatumia mbolea katika kilimo chao kwani sisi tumekuwa tukipima mbolea zote na hii inayozalishwa na kiwanda hiki cha Itracom tumeipima na kuidhinisha kuwa inafaa kwa matumizi ya wakulima wetu na itawapa tija katika kilimo chao," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Itracom, Nduwimana Nazaire, alisema wamepanga kuanza uzalishaji wa mbolea mwishoni mwa mwezi huu.

Nazaire alisema mwishoni mwa mwezi huu wataanza uzalishaji wa tani 200,000 za mbolea na mwakani watazalisha tani 600,000.

"Mbolea yetu tunayozalisha ni rafiki wa udongo kwani inaongeza virutubisho na kurejesha rutuba lakini pia kutokana na kutumia malighafi za hapa nchini bei yake itakuwa chini sana ukilinganisha na zile zinatoka nje ya nchi,"alisema.



# Zanzibar yabuni mbinu mpya chanjo UVIKO -19

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

DAKTARI Mdhamini wa Hospitali ya Wilaya Kusini Unguja iliyoko Makunduchi, Dk. Mohammed Mnyimbi, amesema kuwa utoaji wa huduma ya chanjo ya UVIKO-19 ya kuwafuata wananchi katika harakati zao imesaidia wananchi wengi kuchanja chanjo hiyo.

Amesema awali walikuwa wakitoa huduma hiyo ya chanjo katika hospitali ya wilaya lakini baada ya mwitikio mdogo wa wananchi, walifanya uamuzi wa kuwafuata wananchi katika harakati zao.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake, Makunduchi, mkoa wa kusini Unguja kuhusu uhamasishaji wa chanjo hiyo kwa wananchi.

Dk. Mnyimbi alisema awali watu waliopata chanjo hospitalini hapo ni 300 lakini hivi sasa wamechanja watu 3,400 na kwa wilaya nzima ya Kusini Unguja waliopata chanjo ni 864 ambapo kwa Zanzibar ni wilaya ya pili iliyofanya vizuri kuchanja watu wengi.

"Kliniki ya kutembea imesaidia sana kuongezeka kwa idadi ya watu waliochanja ambapo wataalamu wetu wa afya huwafuata katika harakati zao ikiwemo katika hoteli za kitalii na katika shehia," alisema.

Naye Mkurugenzi Kinga na Elimu ya Afya kutoka Wizara ya Afya Zanzibar, Dk. Ali Nyange, alisema elimu inayotolewa kuhusu chanjo hiyo imesaidia katika mapambano dhidi ya UVIKO-19 na wananchi kupata chanjo ya kujikinga na ugonjwa huo na sasa watu wote waliochanjwa Zanzibar wamefikia 185,000 sawa na asilimia 30 ya malengo.

Alisema ili Zanzibar iwe vizuri ni lazima wananchi wake walindwe dhidi ya maradhi mbalimbali ikiwamo UVIKO-19.

Dk. Nyange alisema pamoja na mafanikio hayo bado watu wengi hawajafikiwa hasa maeneo ya vijijini kwa sababu baadhi ya watu wanaamini chanjo hizo zinaathari licha ya kwamba wote waliochanja hakuna aliyepata tatizo.

"Baadhi ya watu wanazihusisha chanjo za UVIKO-19 na mfumo wa uzazi na mambo mengine ambayo hayana ukweli. Niwasisitize wananchi waendelee kuchanja," alisema.

Alisema chanjo UVIKO-19 ni sehemu ya utaratibu mpya wa dunia kwa sababu watu wote waliokwenda kuhiji Makka wamepata chanjo ya kujikinga na ugonjwa huo.

Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alisema mahujaji wote 1,559 kutoka Zanzibar waliokwenda kuhiji Makka, Saudi Arabia wamechanja chanjo ya UVIKO-19 bila malipo yoyote ili kufanikisha ibada hiyo.

Hata hivyo, alisema wizara ya afya itaendelea kupita nyumba kwa nyumba na sehemu mbalimbali kuwafikia wananchi katika kampeni ya chanjo ya UVIKO- 19 ili kufikia lengo.

Aidha, alizipongeza taasisi binafsi zinazosaidia katika mapambano ya ugonjwa huo ikiwemo kutoa elimu, vifaa tiba na kuiwezesha wizara ya afya kuwapatia wataalamu wa afya kwa gharama za taasisi hizo.



Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, Dk. Mzuri Issa (kulia), akiwasindikiza Maofisa wa Ubalozi wa Norway Tanzania, baada ya kumaliza mazungumzo nao, katika ofisi za chama hicho, Tunguu, Wilaya ya Kati Unguja juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Waziri aomba msaada kufanikisha mapambano vifo vya mama, mtoto

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, ameyaomba mashirika ya Marekani kuisaidia Zanzibar katika kuwapatia vifaa na elimu ya afya ili kutokomeza vifo vya mama na mtoto ifikapo mwaka 2030.

Waziri Mazrui aliyasema hayo jana ofisini kwake Mnazi Mmoja wakati akizungumza na Balozi wa Marekani nchini Tanzania, Donald Wright.

Alisema Zanzibar inatarajia kupunguza vifo vya mama na mtoto na kuhakikisha ina uzazi wa mpango kwa kinamama ili kuzaa watoto wa wenye afya na siha nzuri.

Pia alisema kutokana na changamoto hizo, wizara inajenga hospitali za Wilaya na Mkoa ambazo zitakuwa na sehemu maalum ya akinamama na watoto ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi.

Waziri huyo alisema kupitia jitihada za serikali na wadau mbalimbali wanaosaidia katika sekta ya afya, imefanikiwa kupunguza kwa kiasi kikubwa maambukizi ya mradhi ya malaria na UKIMWI.

Naye Balozi wa Marekani nchini Tanzania, Donald Wright, aliisifu Wizara ya Afya kwa jitihada za kupunguza maradhi ya UVIKO- 19 Zanzibar pamoja na maradhi ya malaria.

Aidha alisema serikali ya Marekani itahakikisha inaendelea kuisadia Zanzibar katika sekta ya afya ili kuondokana na changamoto mabalimbali za maradhi.

# Norway yafurahishwa uwezeshaji wanawake

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UBALOZI wa Norway nchini Tanzania umeeleza kufurahishwa kwake na mafanikio makubwa yaliyoanza kuonekana katika utekelezaji wa mradi wa kuinua ushiriki wa wanawake katika uongozi Zanzibar (SWIL).

Mradi huo unatekelezwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) kwa kushirikiana na asasi zingine za kiraia ikiwamo Jumuiya ya Wanawasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA). Hadi sasa wananchi waliopewa elimu kuhusu ushiriki wa wanawake katika uongozi ni 6,917 wakiwamo wanawake 4,797.

Wakijadili utekelezaji wa mradi huo katika ofisi za TAMWA, Zanzibar zilizoko Tunguu, Zanzibar, maofisa hao wakiongozwa na mwakilishi wa Balozi wa Norway, Bjorn Midthum, walisema kuna mengi makubwa yameonekana kwenye mradi huo kwa kipindi cha miaka miwili tangu kuanza kwake mwaka 2020.

Midthum alisema kuna idadi kubwa ya wanawake waliojitokeza kugombea na kushinda nafasi tofauti za uongozi kuanzia kwenye vyama vya siasa na asasi za kiraia.

Alisema mabadiliko hayo yote anaamini yametokana na nguvu kubwa kupitia mradi huo na hatimaye kwa mara ya kwanza wanawake wengi zaidi wamehamasika na kujitokeza kugombea au kupaza sauti zao.

Pia alisema kupitia vijana maalumu ambao wamepatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo wanajamii (CBS) wamefanya kazi kubwa ya kuhamasisha jamii sambamba na kuongeza kasi ya uwajibikaji kwa viongozi na kuwajibika katika jamii ikiwamo kuwasaidia wananchi katika kutatua changamoto zinazowakabili kwa baadhi ya maeneo.

Alisema awali wakati mradi huo unaanza kulikuwa na changamoto nyingi za wanawake visiwani Zanzibar ikiwemo baadhi yao kushindwa kufahamu kama wao ni sehemu ya jamii na wanapaswa pia kuwa viongozi bali wengi wao waliamini anaepaswa kuwa kiongozi ni mwanamme pekee.

Kwa sasa, alisema changamoto hiyo imeanza kuondoka kwa kasi kubwa ndiyo maana kuna idadi kubwa ya wanawake wanaendelea kujitokeza katika kila chaguzi ziwe za kitaifa au za kichama.

Ofisa huyo alisema mafanikio yote yaliyopatikana kwa miaka miwili ya utekelezaji mradi, yanatokana na nguvu kubwa ya vyombo vya habari ambavyo vinasaidia kupaza sauti za wananchi waliokosa sehemu ya kupaza sauti hizo kwa muda mrefu.

"Tunatoa shukrani zetu za dhati kwa wanahabari wote wanaoendelea kushiriki na kufanya kazi kwenye mradi huu kwa hakika wamefanya kazi kubwa sana inayopaswa kupongezwa na kila mmoja", alisema.

Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar, Dk, Mzuri Issa aliushukuru Ubalozi Norway katika utekelezaji wa mradi huo na kuahidi kuendelea kuwafikia wengi zaidi ili kuleta tija.

Alisema mafanikio hayo ya awali yamekuja kutokana na ushirikiano wa karibu kutoka katika ubalozi huo na anaamini kuwa mafanikio makubwa zaidi yatapatikana na Zanzibar kuingia kwenye historia ya kuwa na idadi kubwa ya viongozi wanawake.



# RAYVANNY HUYOOO! Nani kufuata njia yake?

HATIMAYE mwanamuziki wa Bongo Fleva, Raymond Shabani, maarufu kama Rayvanny ameaga rasmi katika lebo ya WCB, chini ya Diamond Platnumz.

Kuondoka kwake ni sawa na kufuata nyayo za msanii mwingine Harmonize, ambaye alifanya hivyo zaidi ya mwaka mmoja uliopita, tofauti yao ni jinsi walivyonasuka katika kundi hilo lenye wasanii wengi maarufu.

Akiaga katika video ya dakika mbili aliyoitengeneza, Rayvanny ameonyesha heshima kwa WCB na kushukuru mengi aliyofanyiwa hadi hivi sasa kuwa maarufu.

Hata hivyo, CEO wa lebo ya WCB, Diamond Platnumz amebariki safari hiyo huku akionekana kumtakia maisha mapya akiwa na moyo mkunjufu.

Hata hivyo, baadhi ya wachambuzi wamesema kuondoka kwa Rayvanny ndani ya lebo hiyo, kunafungua njia kwa wengine ambao walikuwa wanatamani kufanya hivyo sasa kufuata mkondo.

Lakini Rayvanny ameonekana kuweka zaidi njia ya kiungwana tofauti na Harmonize ambaye wakati akifungasha virago kuliibuka maneno mengi na wakati mwingine kuonekana uhasama wa wazi.

Rayvanny katika salamu zake za kuaga alikuwa na maneno mengi ya hekima huku akitaka kuombewa ili akaanze maisha mengine katika lebo yake aliyoianzisha ya Next level.

"Rayvanny kaonyesha njia ya namna gani msanii unavyotakiwa kuondoka katika uongozi wa zamani hata kama ulikumbana na mabaya. Kafanya uungwana na naamini kuna wengi wanataka kuchukua njia hiyo lakini walikuwa wakitafuta namna ya kupitia," amesema Yusuph Kareem.

BASI SAWA

## Nyota kupambana Shine Festival



Maandalizi ya tamasha kubwa nchini Nyota Shine Festival 2022, yamekamilika tayari kutikisa jiji la Dar Es Salaam Julai 31, katika kanisa la Feel Free Church linalomilikiwa na Masanja Mkandamizaji.

Akizungumza na BT Mkurugenzi wa Nyota Shine, Bahati Simwiche, amesema huo ni msimu mwingine wa tamasha hilo ambalo huwa linafanyika kila mwaka kwenye mikoa tofauti na kuwakutanisha waimbaji nyota kwenye jukwaa moja.

"Maandalizi yamekamilika na tamasha hili linakwenda kusimamisha Jiji la Dar Es Salaam kwa sababu tuna waimbaji wengi ambao tayari wamekubali kushiriki kwenye jukwaa hili, kwahiyo tarehe 31 mwezi juu pale kanisani kwa Masanja Mkandamizaji tunakwenda kuweka historia," amesema Bahati.

## Entujael Msangi acha tu aseme



BAADA ya kufanya vizuri na nyimbo Niko Nuruni na Ushindi lazima, mrembo anayefanya vyema kwenye muziki wa gospo Bongo, Entujael Msangi ametamba kuachia kibao kingine hivi karibuni.

Akizungumza na BT jana, Entujael alisema muda wowote kutoka sasa anakwenda kuachia audio na video ya wimbo wake Nataka Niseme.

" Mwaka huu umekuwa na mafanikio kwenye huduma yangu, nimejipanga muda wowote kutoka sasa niwaletee wapenzi wa muziki wangu wimbo wangu Nataka Niseme ambao naamini utawabariki," amesema Entujael.



# JAY MELODY KALEWA MAPENZI

MSANII wa Muziki wa kizazi kipya, Jay Melody, amesema hawezi kuishi kama hataweza kufikiria suala la mapenzi katika nafsi yake.

Mwimbaji huyo wa kibao cha 'Sugar' amesema kamwe hakuwaza kwamba iko siku anaweza kubadilika asijihusishe katika mapenzi kuliko jambo lolote.

"Binafsi mapenzi yamechukua nafasi kubwa sana kwangu, sikuwahi kufikiria kama nitaweza kubadilika namna hii na yote hayo ni mapenzi". amesema

## Tego la Kijiji: ukijua hili wenzio wajua lile

**Na Adam Fungamwango**

TEGO la Kijiji' ni filamu inayoifunza jamii kuhusu kutotendeana mabaya na kulipizana visasi. Inaifundisha jamii kuchukua hatua zinazokubalika, zilizowekwa na kukubaliwa na wote kama litatokea tatizo na si kujiamualia au kuchukua sheria mkononi.

Imechezwa na wasanii Mohamed Fungafunga, maarufu kama mzee Jengua (marehemu), Ibrahim Kirangi, Rahma Mussa, Said Mpoto, mzee Msisiri wa Msisiri, mzee Korongo na wengineo.

Inaanza kwa kuonyesha Mzee Msisiri akienda nyumbani kwa mzee Jengua kulalamika kuhusu kumega shamba lake na kumuuzia mtu mwingine.

Mzee Jengua anakuwa mkali kama mbogo akisema ameuza sehemu yake na si ya Mzee Msisiri. Ugomvi huo unafikishwa kwa Mwenyekiti wa Kijiji, mzee Kongoro, lakini unamuwia vigumu kutokana na ubishi wa asili wa wazee hao wawili.

Ni kama kidonda kilichowekwa chumvi na pilipili, Kipe binti wa Mzee Jengua anapobanwa ujauzito.

Anapobanwa na mama yake anamtaja Ndolo mtoto wa mzee Msisiri kuwa ndiye aliyempa ujauzito.

Kibaya zaidi ni kwamba msichana huyo ni mchumba wa mtu, ambaye baada ya kuwasili kijijini kutoka mjini anakutana na habari hiyo mbaya, anakwenda kudai mahari yake ambayo tayari ameshatoa nusu.

Ni kasheshe juu ya kasheshe. Ugomvi wa wazee hao wawili wa kunyang'anyana mashamba, sasa unageukia kwa watoto wao.

Mzee Jengua alipopata habari hiyo, aliwaka na kumcharaza bakora, binti na mama yake, huku akiahidi kufanya kitu kibaya kwa familia ya Msisiri.

Akaenda kwenye mti mmoja mkubwa na kuomba mizimu imsaidie kulipiza kisasi cha mzee Msisiri. Akatokea mzimu mbaya wa kike, ambao ulianza kuua watu hovyo kijijini.

Shetani hilo halikuchagua, si wale waliofanyiwa ubaya, waliofanya na ambao hawahusiki kabisa.



Likaanzia kuwatokea na kuwadhuru watu wa ukoo wa Msisiri, baadaye ya mzee Jengua pia.

Hali ikazidi kuwa mbaya. Mzee Msisiri akaenda kwa mganga wa kienyeji aitwaye Kantangaze. Yeye akabainisha ukweli wote yanayotokea yamesababishwa na mzee Jengua.

Hakuwa na la kufanya, badala yake akakubali na kuomba msamaha kwa sababu mzimu badala ya kufanya kazi iliyoombwa ukawa unaadhibu wote.

Msisiri akakubali msamaha wa mzee Jengua. Msisiri akaahidi kuwa atamtunza binti wa Jengua hadi atakapojifungua kwa sababu ni damu yao.

Wanakijiji wanaungana na mganga Kantangaze kusaka mzimu unaowasumbua kwa kuua, kujeruhi na kupiga watu, hadi wakauangamiza, kijiji kikarejea kwenye hali ya amani.





## Mlela mbona unajisifu?


MWIGIZAJI wa filamu Yusuph Mlela, amejinasibu kuwa yeye ndio 'msanii wa kuigwa kwa vijana wengi wanaochipukia kwenye tasnia hiyo kwa sababu amewafanya wafanye filamu kwa kuwashauri.

"Kwa hawa vijana wanaokuja sasa hivi nimewahamasisha wengi sana, ukiangalia asilimia nyingi nimewafanya kuingia katika game na mimi ndio mtu wao wa mfano, kwangu ni kitu kizuri kuna muda nakutana nao nawapa ushauri".

Pia Yusuph Mlela amesema tasnia ya filamu bado inahitaji watu wengi kwa sababu waliopo ni wachache.

## WALIOFARIKI MWEZI JUNI KAMA MICHAEL

**Na Adam Fungamwango**



JUNI 25 mwaka huu, dunia iliadhimisha miaka 13 ya mwanamuziki maarufu duniani Michael Jackson, aliyefariki mwaka 2009 huko Califonia nchini Marekani.

Katika kumbukumbu hiyo, hapa nchini Tanzania tutawakumbuka wanamuziki wa dansi waliofariki mwezi kama huo kwenye miaka tofauti.

Wakati nchini Marekani mwezi Juni waliadhimisha kifo cha staa huyo wa dunia aliyezaliwa nchini mwao, nchini Tanzania tutawakumbuka baadhi ya wanamuziki maarufu kabisa nchini ambao walifariki mwezi kama huo na kuacha majonzi makubwa kwa familia zao, pamoja na mashabiki wa muziki wa dansi nchini.

**Abel Bathazar- 6 JUNI 1994**

Juni 6 mwaka 1994 alifariki mwanamuziki maarufu na mpiga gitaa ongozi la solo, Abel Bathazar.

Akiwa kwenye bendi ya Magereza nyimbo yake ya mwisho maarufu kupiga solo ilikuwa ni 'Ashura' ulioimbwa na mwimbaji wa kike, Nana Njige ambaye naye ni marehemu.

Akitokea Kilosa, alijiunga na NUTA Jazz na kupiga karibuni nyimbo zote za bendi hiyo kwa mtindo wa Msondo Ngoma hadi alipohama mwaka 1977 kwenda kuunda bendi ya Dar International.

Mwaka mmoja baadaye akiwa na kundi la Dar International na baadhi ya Msondo waliunda kundi la Mlimani Park Orchestra.

**Suleiman Mbwembwe-12 JUNI 2004**

Juni 12, 2004, tasnia ya muziki ilimpoteza muimbaji wa sauti ya kwanza kali nchini Suleiman Mbwembwe. Wakati anafariki alikuwa kwenye kundi la Msondo Ngoma Music Band.

Alipitia bendi mbalimbali ikiwemo Tanzania Stars na baadaye Juwata Jazz Band akiwa na kina TX Moshi waliofanya mambo makubwa kwa kutunga na kuimba nyimbo nyingi.

Mwanzoni mwa miaka ya '90 alijiunga na Vijana Jazz na kurejea Msondo mwanzoni mwa miaka ya 2000.

**Athumani Momba-18 JUNI 2005**

Mwaka mmoja baada ya kifo cha Mbwembwe, tena ikiwa mwezi Juni, siku sita tu baada ya kuadhimisha mwaka mmoja wa kifo chake, alifariki mwanamuziki mwingine wa Msondo, Athumani Momba aliyeanza kujulikana kwenye bendi ya Dar International.

Muda mfupi baadaye aliondoka Vijana na kujiunga na Bima Lee ambako aliimba sauti ya kwanza kwenye karibuni nyimbo zote akishirikiana na Shaaban Dede.

Alichukuliwa na Msondo mwaka 1990, lakini baadaye alirejea tena Vijana, kabla ya kurejeshwa tena Msondo ambako alihudumu hadi alipofariki dunia.

**Harila Tongolanga-4 JUNI 2017**

Huyu ni mtunzi na mwimbaji maarufu zaidi wa nyimbo za Kimakonde. Alianza kujulikana mwishoni mwa miaka ya '80 alipotoa kibao cha 'Kila Munu Ave na Kwao' akiwa na CTU Les Mwenge ya Arusha.

Baadaye alianzisha bendi ya Makondeko Six band ambayo ilitamba na nyimbo kama 'Kila Munu Ave na Kwao' ikiwa na sehemu ya pili hadi ya nne, 'Saidaru', na nyingine nyingi. Harila pia alikuwa na kundi la zing zong la Bana Mwambe akiwa na akina Tx Moshi, lakini pia akiwa na mialiko mingi nchini Msumbiji. Alifariki dunia Juni 17, 2017.

**Shaaban Dede-6 JUNI 2017**

Siku mbili baadaye baada ya kufo cha Tongolanga, mwanamuziki mwingine maarufu nchini alifariki dunia kwenye Hospitali hiyo hiyo ya Muhimbili. Wanamuziki walikuwa wakienda kuwaangalia wagonjwa wote wawili. Lakini kwa bahati mbaya wote walifariki kwa siku mbili tofauti. Dede ambaye naye alifariki mwezi kama huo, tarehe 6 Juni 2017, ni mtunzi, mwimbaji wa sauti ya kwanza na ndiye aliyekuwa akiziba pengo la Hassan Rehani Bitchuka kila alikokwenda.

Ni mmoja wa wanamuziki waliopigia bendi nyingi nchini kama Juwata Jazz, DDC Mlimani Park, OSS, Bima Lee. Alifariki akiwa kwenye bendi ya Msondo Ngoma.



# Kholeo, Tristan kupata mtoto wa pili

NYOTA wa kipindi cha maisha ya ukweli wa Marekani, Khloé Kardashian, anatarajia mtoto kupitia mwanamke.

Kulingana na mtandao wa Pagesix, wa ziada na Tristan Thompson.

Kulingana na PageSix, chanzo karibu na familia ya Kardashian kilifichua kuwa Khloe na mume wake ambaye wametengana, Tristan Thompson, wanatarajia mtoto wao wa pili kupitia kwa mwanamke huyo wa siri.

"Tunaweza kuthibitisha kuwa True atakuwa na kaka yake ambaye alitungwa mimba mnamo Novemba. Khloe anamshukuru sana kupata baraka hizo nzuri," chanzo kilifichua.



## Portable kweli unayoyasema?

RAPA mtukutu kutoka mitaa ya Nigeria, Habeeb Okikiola, maarufu kama Portable, amefichua kuwa chama cha All Progressive Congress (APC) kimemlipa ili kumpigia debe mgombea wake wa urais, Bola Tinubu.

Hapo awali mwimbaji huyo alikosolewa vikali kwenye mitandao ya kijamii baada ya kutangaza kuunga mkono APC katika uchaguzi wa ugavana wa Jimbo la Osun.


Katika video iliyowekwa kwenye ukurasa wake wa Instagram, mwimbaji huyo wa 'Zazuu' aliwaomba Wanigeria kumpigia kura Tinubu katika uchaguzi wa urais wa 2023.

## Oprah ampoteza baba yake

MTANGAZAJI maarufu kutoka Marekani, Oprah Winfrey, amempoteza baba yake mzazi, Vernon Winfrey, ambaye amefariki wiki hii.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Winfrey ambaye ni bilionea amesema amehuzunishwa kumpoteza baba  na rafiki yake.

"Chini ya wiki moja iliyopita tulimheshimu baba yangu katika uwanja wake wa nyumba. Rafiki yangu na mwimbaji wa nyimbo za injili Wintley Phipps alimsalimia kwa wimbo, sasa anashindwa kuongea tena," aliandika





## Davido aapa kutobadilika

MWANAMUZIKI nyota kutoka Nigeria, Davido amesema kwamba ana hofu mashabiki wake wanaweza kuhisi mafanikio na utajiri alionao unaweza kumbadilisha kitabia.

Msanii huyo bilionea alitumia muda wake katika ukurasa wake wa Instagram, kueleza kwamba kamwe hawezi kubadilika licha ya kuwa tajiri.

"Pesa na mafanikio niliyokuwa nayo kamwe haviwezi kunibadilisha, siwezi kubadilika kwa kila kitu kwangu ni jambo lenye athari kwangu," amesema Davido

## Agupa kama kweli umelenga

MWIGIZAJI nguli kutoka Nollywood, Kenneth Aguba, amefichua kwamba amempata binti mbichi kutoka Israel ambaye anataka kumuoa.

Kulingana na Aguba, mwanamke huyo bikira si kwamba anatarajia kufunga naye ndoa, pia anafurahi kutoka katika taifa hilo teule.

Mwigizaji huyo ambaye alianzia maisha ya mtoto wa mitaani, amepata mafanikio makubwa katika tasnia hiyo na kumfanya kuwa miongoni mwa watu maarufu nchini Nigeria.



MAKALA

# CHT inavyompambania mtoto yatima aliyezaliwa na tatizo la kichwa kikubwa

Na Sabato Kasika

ULEMAVU wa kichwa kikubwa na mgongo wazi ni mojawapo ya changamoto inayokabili watoto wengi nchini.

Tatizo hilo ambalo linazidi kuwa kubwa, linasababisha baadhi ya wazazi kujiua na hata wanaume kukimbia familia zao.

Katika mazingira hayo, wengine wanakwenda kwa waganga wa kienyeji wakiamini watoto wao wamelogwa, hali ambayo inaonyesha kuwa bado elimu ya kutosha inahitajika ili angalau kupunguza imani hiyo.

Mfano, ni tukio la hivi karibuni lililotokea mkoani Njombe, ambako mwanamke aliyetajwa kwa jina la Sarah Lukelema alijinyonga baada ya kujifungua mtoto mwenye ulemavu wa kichwa kikubwa na mgongo wazi.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Njombe, Hamis Issa, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo mwishoni mwa Mei mwaka huu, huku akitoa wito kwa wakazi wa mkoa huo kuacha matendo ya unyanyapaa.

Tukio la mwanamke huyo kujinyonga kwa sababu ya kuzaa mtoto wa aina hiyo, liliwasukuma viongozi wa Taasisi ya Child Help Tanzania (CHT) kufunga safari hadi Njombe kumchukua mtoto huyo.

Katika mazungumzo yake na gazeti hili, Mkurugenzi CHT, Hakim Bayakub anasema, kwa sasa mtoto huyo yupo Taasisi ya Mifupa ya Hospitali ya Taifa Muhimbili (MOI), kwa ajili ya kupatiwa huduma za kimatibabu.

Anasema, umefika wakati jamii iachane na mila potofu ili kuwezesha watoto wanaozaliwa wakiwa na ulemavu waweze kupata huduma za afya.

**NINI KIFANYIKE?**

Mkurugenzi huyo anasema, elimu zaidi kuhusu chanzo cha ugonjwa huo ni muhimu iendelee kutolewa zaidi hasa maeneo ya vijijini ambako ndiko kwenye changamoto kubwa ikiwamo umaskini wa kipato.

"Sisi kama taasisi tumekuwa tukitoa elimu, lakini ni vyema wadau mbalimbali wakaunga mkono juhudi hizi, ili kusaidia jamii kutambua kuwa ulemavu huo si uchawi bali unaweza kuepukika,"anasema Bayakub.

Anasema, inawezekana hata tukio la mwanamke aliyejinyonga huko Njombe likawa limesababishwa na ukosefu wa elimu na wakati mwingine umaskini wa kipato na hivyo kuamua kujiondoa uhai.

"Labda alienda hospitali akaambiwa gharama za huduma kwa mtoto akaona ni kubwa, au aliona ni uchuro ama alikimbiwa na mume akaona ni bora akatishe maisha yake kuliko kukaa pekee yake na mtoto huyo," anasema.



Viongozi wa Taasisi ya Child Help Tanzania baada ya kumpokea mtoto huyo katika kituo cha mabasi cha Magufuli Dar es Salaam. Kushoto ni Ofisa Mawasiliano wa taasisi hiyo Milton Byemerwa, Mkurugenzi Hakim Bayakub, bibi wa mtoto huyo na Meneja wa Program, Sifa John. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**



Ofisa Mawasiliano wa taasisi hiyo, Milton Byemerwa akiwa na mtoto huyo.

Bayakub anasema, taasisi yake imekuwa ikizunguka maeneo mbalimbali nchini kutoa elimu, na kwamba wako mbioni kuzunguka wakianzia ngazi ya mkoa, wilaya, tarafa, kata, mtaa, vijiji na vitongoji.

"Tunapanga ratiba hiyo huku tukiendelea kuratibu huduma za mtoto ambaye tulimtoa Njombe baada ya mama yake kujinyonga, kwani tumewaachia wataalam wa afya wafanye kazi yao," anasema.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa CHT, Militon Byemerwa, anasema taasisi hiyo ni mdau mkubwa katika tiba za watoto wenye ulemavu huo, hasa kwenye eneo la ufadhili wa vifaa tiba ndani ya taasisi ya MOI ambayo ni mnufaika.

"Tunafadhili mirija ya kuratibu maji katika ubongo kwa wenye kichwa kikubwa, ama za upasuaji kwa wenye mgongo wazi

> **Katika kila watoto 1000, watoto watatu kati yao wanazaliwa wakiwa na ulemavu huo, takwimu za watoto wanaozaliwa kila mwaka hufikia takribani milioni 2, hivyo watoto 6,000 kila mwaka huzaliwa na tatizo hilo," anasema.**

na kikubwa, mirija ya kusaidia wasio na hisia za haja kubwa na ndogo,"anasema.

Anasema, mirija hiyo ni maalum ambayo inahakikisha maji hayawi mengi kichwani, kwa kuwa yakiwa mengi kinaweza kuongezeka, hivyo wanajitahidi kuhakikisha huduma hiyo inapatikana.

Anafafanua kuwa Taasisi ya Child Help Tanzania inatoa elimu kwa umma kuhusu kinga ya tatizo hilo na matibabu yake, lengo likiwa ni kuona jamii yenye afya bora bila ulemavu wa kichwa kikubwa na mgongo wazi.

"Kuzaa mtoto mwenye kichwa kikubwa na mgongo wazi lilitugusa sana, ndiyo maana tukafunga safari kufuata mtoto ili awe karibu na huduma za afya," anasema Byemerwa.

**CHANZO CHA ULEMAVU**

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu anasema, chanzo chake ni ukosefu wa madini ya foloki asidi, anawaagiza waganga wakuu wa mikoa na wilaya kuhakikisha yanapatikana kirahisi katika ngazi zote za kutolea huduma za afya.

Anafafanua kuwa tatizo la watoto kuzaliwa na kichwa kikubwa na mgongo wazi linaweza kuzuilika, kwa kuwa linatokana na ukosefu wa madini hayo, ambapo anataka yapatikane hadi kwenye zahanati.

"Wanawake walio kwenye umri wa kuzaa au wanaopanga kupata watoto, wale vyakula vyenye kuongeza madini ya foliki, ili kuongeza kinga ya kumkinga mtoto dhidi kuzaliwa akiwa na ulemavu huo," anasema Ummy.

Anasema, takwimu zinaonyesha kuwa, katika nchi tano za Afrika zenye watoto walio na ulemavu huo, Tanzania inashikia nafasi ya tano ikiwa imetanguliwa na nchi za Argelia na Ethiopia.

"Katika kila watoto 1000, watoto watatu kati yao wanazaliwa wakiwa na ulemavu huo, takwimu za watoto wanaozaliwa kila mwaka hufikia takribani milioni 2, hivyo watoto 6,000 kila mwaka huzaliwa na tatizo hilo," anasema.

Waziri Ummy anawataka madaktari, wakunga na wauguzi pindi wanapozalisha na kuona mtoto mwenye dalili za kichwa kikubwa na mgongo wazi, watoe rufaa haraka, ili watoto waweze kupata huduma mapema.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Vinywaji, misosi ya zamani ilivyogeuka adimu

## •Togwa, chibuku navyo vilitikisa

Na Adam Fungamwango




LEO unamuona mtu anatembea na chupa yake ya maji. Anakunywa bila wasiwasi. Amenunua dukani, wala hamuulizi mtu.

Anaweza kutoka na maji yake kwenye chupa kutoka mkoa mmoja mpaka mwingine, au sehemu moja mpaka nyingine. Anaposikia kiu anakunywa. Anajisikia hamu anakunywa pia.

Unaanza kukumbuka enzi hizo. Miaka ya kuanzia mwishoni mwa miaka ya 1990 kurudi nyuma. Hakukuwa kabisa na maji ya chupa.

Yoyote aliyekuwa na kiu kama yupo mtaani anatembea alilazimika ama kutafuta sehemu ambayo ina mgahawa na kwenda kuomba maji, au kugonga hodi kwenye nyumba ya mtu.

Siyo wakubwa tu, hata watoto ambao wanakuwa wametoka kwenye michezo yao ikiwemo mpira wa miguu, walikuwa wakigonga hodi kwenye majumba ya watu na kuomba maji.

Mwenye nyumba anatoka na glasi moja pamoja na jagi na kuwapa.

Hayo ndiyo yalikuwa maisha ya zamani. Maji ilikuwa ni mpaka uingie hotelini au uombe kwenye nyumba za watu. Hakuna duka lolote lililokuwa linauza maji ya kwenye chupa. Na wala hayakuwepo.

Kwa wakati huo vinywaji dukani vilikuwa ni soda tu. Na kwa wakati huo kunywa soda halikuwa jambo la kawaida. Kwa mtoto ukinywa ni lazima ukasimulie.

Mara nyingi soda ilinywewa kwenye wakati wa hafla mbalimbali, matukio ya kijamii, ikiwemo sherehe mbalimbali kama ubatizo, kipaimara, maulidi, harusi.

Familia nyingi ziliweza kumudu kununua soda siku ya sikukuu, hapo ndipo utakapoona watoto na familia nzima inakunywa soda. Kama ni siku za kawaida basi akija mgeni ndiyo ananunuliwa. Watoto wote mnatimuliwa ili msimuombe kwa sababu haikuwa jambo lililozoeleka kunywa soda.

Siku hizi soda zinashinda kwenye friji, watoto na wakubwa wanakunywa wanapojisikia tu. Kweli kila kitu na zama zake. Kijana wa sasa akisikia hivi atashangaa sana.

Ukiacha kinywaji hicho ambacho kilikuwa adimu mno, kinywaji kilichokuwa maarufu sana wakati huo ni togwa.

Kwa wale wa vijijini walikunywa togwa ambalo lilitokana na ulezi, mtama na hata mahindi wakati wa kutengeneza pombe.

Kabla halijachachuka na kuwa pombe inakuwa togwa tamu ambayo kila mtu hata watoto hunywa na kuburudika kwa sababu inakuwa haina kilevi.

Kwa wale wa mikoa mikubwa, hasa ya Pwani, kulikuwa na togwa lililokuwa likitengenezwa na akinamama kwa kutumia mtama.

Kinamama hao walilitengeneza kwa kuweka kwenye chupa za soda na kufunga kwa kutumia vipande vya magazeti kwenye mdomo wa chupa kama picha inavyoonyesha.

Ilikuwa si ajabu kupita kwenye nyumba mbalimbali na kukuta kiti cha marimba, au kigoda kikiwa na beseni au sufuria lililokuwa na maji, halafu chupa za togwa zikiwa ndani yake.

Yoyote anayetaka kunywa anaita, na muuzaji ambaye nimesema wengine wao ni akinamama watu wazima, atatoka na kukuuzia.

Unywaji wake ilikuwa ni wa aina moja. Kabla ya kunywa kuna kitu ilikuwa ni lazima ukifanye.

Ni lazima kwanza utikise chupa ili yale machicha yake yasibakie kwenye chupa, kwa sababu ladha ya togwa ni yale machicha yenyewe.

Atatikisa kama mtu anayetaka kunywa dawa, na atakunywa kwa raha zake. Baadaye atakweka chupa yake kwenye sufuria au beseni baada ya kulipa pesa na kuondoka.

Miaka hiyo si maduka mengi yalikuwa na freji, hivyo watu wengi wanapopatwa na kiu, wakitaka kinywaji cha baridi, kuna wafanyabiashara njiani ambao walikuwa wanauza juisi za ukwaju, lakini kwa wakati huo yalijulikana kama 'maji ya barafu.'

Wanakuwa na ndoo na maji yenye ukwaju, iliyosheheni mabonge ya barafu, na mteja akifika atamiminiwa kwenye glasi. Hii ndiyo ilikuwa njia pekee ya kutia kitu cha baridi kooni.

Kinywaji kingine maarufu wakati huo kilichokuwa na kilevi ni pombe aina ya chibuku. Asili yake ni nchini Zambia. Hapa nchini maeneo ya Ubungo kulikuwa na kiwanda cha kutengeneza pombe hiyo.

Ilikuwa maarufu mno kwenye maeneo mbalimbali wanayouza. Kwenye mabaa wanayouza bia hazikuwepo sana, badala yake ilikuwa inauzwa zaidi kwenye maeneo ambayo wenyewe waliita klabu au vilabu. Wakati huo umaarufu wake ilijulikana kama 'kilabu cha pombe'.

Huko ndiko kulikuwa na wateja wa chibuku ambayo ilikuwa ikiboreshwa kila miaka ilivyozidi kusonga mbele.

Kwanza ilikuwa ikiletwa kwenye malori kama ya maji, au mafuta na kumiminwa kwenye matanki vilabuni, kabla ya kupimwa kwenye makopo ya plastiki kulingana na ukubwa wake kwa matakwa ya mteja.

Teknolojia ilipokua, chibuku ikaanza kutengenezwa na kuwekwa kwenye vifungashio kama vile maboksi ya plastiki kama vile maziwa, na pia chupa, mpaka pale kiwanda kiliposhindwa kujiendesha, kikafa kifo cha asili.

Kuna vyakula vingi ambavyo vilikuwapo sana wakati huo ambavyo kwa sasa ama vimekuwa adimu au havipo kabisa ni mabumunda.

Hata hivyo kwa vijana wa mjini hasa Dar es Salaam, mabumunda yalijulikana kwa jina la bisi.

Ni mahindi yaliyokaangwa na kupasuka kama tunavyoona sasa biashara hiyo kwenye vituo vya mabasi na kuwekwa kwenye mifuko ya nailoni, lakini bisi za wakati huo huwekwa sukari na kufinyangwa kama tonge la ugali. Ile sukari ambayo nayo imekaangwa, ikayafanya mahindi hayo kushikana na kuwa kama umbile la mpira wa kitenesi au zaidi ya hapo kama inavyoonekana kwenye picha.

Vyakula vingine ni wanga, pepeta, ukwaju wa kizungu, matunda ya ng'ongo ambayo hutumika pia kutengeneza pombe ya amarula.

Pia kwa sasa kuna uhaba wa vitafunwa kama visheti na mikate ya kumimina.

Katika utafiti wangu mdogo niligundua kuwa zamani, vitafunwa kama maandazi, vitumbua, chapati ambavyo hadi leo vimebaki kuwa vitafunwa vikuu hadi vizazi vya sasa wapishi na wauzaji wake walikuwa ni wasichana na akinamama wenye umri wa wastani.

Lakini mikate ya kumimina iliuzwa zaidi na wanawake wenye umri mkubwa, yaani mabibi.

Kwanza mikate ya kumimina ambayo inatengenezwa kwa kutumia mchele na kufunikiwa na moto juu kama wali, pamoja na ufundi mwingine haikuwa na wauzaji wengi.

Kwenye mauzo ya vitafunwa unaweza kumkuta mtu mmoja tu anauza naye ni bibi. Au wakati mwingine wateja walilazimika kumfuata mtu mzima huyo nyumbani kwake.

Hadi leo hii ni rahisi sana kupata vitafunwa vyote, lakini siyo mikate ya kumimina.

Je uandaaji wake na upikaji wake ni mgumu kwa wasichana au kinamama kwa umri wa wastani?

Kwa nini wazee walikuwa ndiyo wapishi wakubwa wa mikate ya kumimina? Wao walikuwa na ufundi au ujuzi gani wa ziada kuliko wanawake walio na umri mdogo kuliko wao?

Je, ilitumia muda mrefu na umakini kutengeneza kuliko vitafunwa vingine?

**Tuma meseji 0716 350534**






## Waziri Mkuu Sri Lanka aapishwa urais

**COLOMBO,** SRI LANKA

WAZIRI Mkuu wa Sri Lanka, Ranil Wickremesinghe, ameapishwa kushika nafasi ya rais, wakati waandamanaji wakiendelea kuminimika mitaani wakilalamikia kudorora kwa uchumi na kumtaka ajiuzulu.

Ranil anajaza nafasi ya Gotabaya Rajapaksa, ambaye amekimbilia taifa la Singapore,baada ya waandamanaji kuvamia makazi yake.

Waandamanaji wamekuwa wakipuuza hali ya dharura iliyotangazwa wakisherehekea kujiuzulu kwa Rajapaksa.

Sri Lanka inapitia wakati mgumu wa kiuchumi, wakati kuna uhaba wa chakula, mafuta na bidhaa nyingine muhimu.

Shughuli ya bunge ya kumchagua rais mpya itaanza kesho, wabunge wakitarajiwa kupiga kura juma lijalo kumchagua rais.

Kutokana na wabunge wengi kuwa wa chama tawala, huenda wakamchagua Wickremesinghe , ambaye ana uhusiano wa karibu na familia ya Rajapaksa. **RFI**

## Liz Truss apata uungwaji mkono

**LONDON,** UINGEREZA

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Uingereza Liz Truss, amepata uungwaji mkono na idadi kubwa ya wabunge kushika nafasi ya waziri mkuu.

Truss anaungwa mkono na mwakilishi wa Uingereza katika mazungumzo ya Brexit, David Frost na mbunge Suella Braverman ambao ni maarufu katika siasa za nchi hiyo.

Waziri huyo alipata kura 64 katika duru ya pili ya uchaguzi wa viongozi wa chama cha kihafidhina uliofanyika juzi na aliahidi kuinua uchumi wa nchi hiyo ifikapo mwaka 2024.

Waziri wa zamani wa fedha Rishi Sunak, aliongoza kwa kura 101, akifuatiwa na naibu waziri wa biashara Penny Mordaunt aliyepata kura 83.

Gazeti la The Times limeripoti kuwa Waziri Mkuu Boris Johnson amewahimiza wagombea walioshindwa kutomuunga mkono Rishi.

Johnson alifanya mazungumzo na wagombea walioshindwa na kuweka wazi kwamba Rishi Sunak hapaswi kuchaguliwa kuwa waziri mkuu.

Gazeti hilo limenukuu chanzo kilichosema kuwa Johnson anampigia upatu Truss kurithi nafasi yake **DW**

# Biden atembelea Jerusalem Mashariki

**JERUSALEM,** PALESTINA

RAIS wa Marekani Joe Biden, anaendelea na ziara ya mashariki ya kati na jana amekwenda mji wa Jerusalem mashariki.

Kiongozi huyo aliitembelea hospitali moja na kuahidi dola milioni 100 kwa ajili ya kuzisaidia.

Hata hivyo, waandamanaji kadhaa wanaoiunga mkono Palestina, walijitokeza Jerusalem Mashariki kabla ya rais huyo hajatembelea eneo hilo. Waandamanaji hao walibeba bendera za Palestina na mabango ya picha za mwandishi wa habari Mmarekani aliyekuwa na asili ya Palestina wa kituo cha televisheni cha Aljazeera Shireen Abu Akleh aliyeuawa hivi karibuni katika ukingo wa magharibi wakati akiripoti kuhusu uvamizi wa jeshi la Israel katika eneo hilo la Wapalestina.

Jana Biden alizuru hospitali ya Augusta Victoria iliyoko Jerusalem Mashariki ambayo inatoa huduma kwa Wapalestina na kuahidi msaada wa ziada wa dola milioni 100 kwa ajili ya kusimamia shughuli za hospitali za eneo hilo.

Baada ya kutembelea hospitali hiyo, alikwenda Ukingo wa Magharibi kukutana na Rais wa Mamlaka ya Wapalestina, Mahamood Abbas ambako ni kituo cha mwisho cha ziara yake katika eneo hilo kabla ya kuelekea Saudi Arabia.

Rais huyo wa Marekani hakutoa mwelekeo wowote wa wazi wa kuzirudisha kwenye meza ya mazungumzo ya amani Palestina na Israel.

Hata hivyo, alisema Wapalestina na Waisrael wanastahili kuwa na hali sawa ya uhuru,usalama maendeleo na heshima na kupata huduma ya afya pale inapohitajika.

Katika hatua nyingine, Biden alitangaza msaada wa dola milioni 201 kwa ajili ya shirika la Umoja wa Mataifa la kuwasaidia wakimbizi Wakipalestina pamoja na fedha nyingine za kusimamia miradi mingine.

**DW**



Wanawake wa Kiturkana wakiwa wamebeba kuni wakipita karibu na mifupa ya mnyama aliyekufa kutokana na ukosefu wa chakula katika eneo la Loiyangalani.Eneo la Kaskazini mwa Kenya kunakabiliwa na njaa baada ya kukosa mvua kwa muda mrefu. **PICHA: AFP**

# Hungary yaionya Ulaya kukimbilia vikwazo kama silaha kwa Russia

**BUDAPEST,** HUNGARY

WAZIRI Mkuu Hungary, Viktor Orban, amesema hatua ya Umoja wa Ulaya kuiwekea vikwazo Russia ni sawa na mwiba wa kujidunga mwenyewe.

Alionya iwapo vikwazo hivyo havitaondolewa, uchumi wa Ulaya utaporomoka zaidi.

Katika mahojiano na kituo kimoja cha redio, Orban ambaye tangu mwanzo amekuwa akipinga vikwazo hivyo alisema vikwazo dhidi ya Russia haviisaidii Ukraine na kwamba vina athari ya moja kwa moja kwa uchumi wa Ulaya.

Waziri Mkuu huyo amekiri kuwa Ukraine inahitaji msaada, licha ya viongozi wa umoja huo wanapaswa kufikiria upya juu ya mikakati yao kwani kinyume na walivyotarajia, uchumi wa Ulaya umeendelea kuporomoka bila ya kuidhoofisha Russia.

Usambazaji wa gesi barani Ulaya umepungua na gharama ya bei ya mafuta imepanda maradufu duniani kote tangu Russia ilipoivamia Ukraine mnamo Februari 24.

Wakati huo huo, Waziri wa fedha wa Marekani Janet Yellen, ametoa mwito kwa kundi la mataifa yaliyoendelea kiviwanda duniani G-20 kuchukua hatua za haraka kushughulikia mparaganyiko katika usambazaji wa chakula duniani.

Alisema tatizo hilo limechochewa na vita vya Russia nchini Ukraine, na hatua hiyo itaepusha kupanda kwa bei za bidhaa katika soko la kimataifa na kuzuia wafanyibiashara walaghai kuhodhi vyakula.

Akizungumza katika mkutano wa mawaziri wa fedha wa G-20 nchini Indonesia, Yellen alisema nchi zinapaswa kutoa usaidizi wa kifedha kwa wale wanaohitaji badala ya kutoa ruzuku za muda mfupi.

Alizihimiza nchi wanachama kuongeza matumizi yao katika kushughulikia changamoto za uhaba wa chakula, mabadiliko ya tabia nchi na misukosuko ya kiuchumi kutokana na janga la ugonjwa wa COVID-19.

Waziri huyo wa fedha wa Marekani alisema kuwa rais wa Russia Vladimir Putin anatumia suala la chakula kama silaha ya vita, akitolea mfano wa uharibifu wa vifaa vya kilimo na kufungwa kwa bandari katika bahari nyeusi.**DW**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI**
**INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

## KUPOTEA KWA CHETI



**HASSAN ABDINI MREMA** anatangaza kupotelewa na cheti cha chuo chenye index namba **SMMUCO BBA-Ed12/133** kilichotolewa na chuo cha **STEFANO MOSHI MEMORIAL UNIVERSITY** (constituent collage of tumaini university makumira) kozi ya **BACHELOR OF BUSINESS ADMINISTRATION WITH EDUCATION** mwaka 2015,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Polisi taarifa **KIL/MOS/RB/269137/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**HENRY DENNIS MILANZI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2354-0042** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya **EAGLES BOYS SECONDARY** mwaka 2012,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Polisi taarifa **MDL/RB/2207/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**GASPERY DEMITILIUS LWENA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2299-0036** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia KITWIRU SEKONDARI mwaka 2011. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/KIG/RB/278306/2022.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**RASHID HAMAD ABDALLA** anatangaza kupotea kwa cheti cha chuo chenye namba ya usajili **UG2016986415** kilichotolewa na OPEN UNIVERSITY OF TANZANIA mwaka 2019. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/CEN/RB/280888/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MOGELA SHABANI** anatangaza kupotelewa na cheti cha UALIMU DARAJA LA III C kozi ya UALIMU yenye namba ya usajili **MOR/08/227** kilichotolewa na CHUO CHA UALIMU MOROGORO mwaka 1980,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Polisi taarifa **MOR/PS/B.I/35/VOLXCIX/20**

## KUPOTEA KWA CHETI



**PETER ALOYCE SARON** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.1757/0611** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya **BENDEL MEMORIAL SECONDARY** mwaka 2016,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **DAR/CHU/RB/280857/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA MJINI MOROGORO KITUO CHA MJINI MKOA WA MOROGORO**

**USIMAMIZI WA MIRATHI NA…40../2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: JAMILA DAUD NYABU WA MSAVU KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA: REHEMA JOHN LYIMO**

## TANGAZO

**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 29/07/2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya narehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

Imetolewa Tarehe 15/07/2022

15 Mwezi 7 Mwaka 22
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NDUGU: ABUBAKAR MOHAMED KABEYA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 406 DAP** aina ya **TOYOTA IPSUM** yenye rangi ya golden (dhahabu), kwa yoyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu naye kwa kumbukumbu **MWA/NYA/RB/206629/2022**

***Uza,***
***Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***
***Tupigie***
***0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MGENI wa ajabu anatokea kwenye kijiji cha Semwanza, Lugoba mkoani Pwani. Anakotoka hakujulikani. Watu wote wanamwogopa. Ni kwa sababu hawamjui. Msichana Siwatu anajitolea kumsaidia mgeni huyo. Kwa kufanya hivyo, anabezwa kwa maneno mengi ya kejeli kwa kumsaidia mtu asiyemjua ambaye anaweza kuwa hatari kwa kijiji. Baadhi ya viongozi wa kijiji waliungana na wanakijiji kutaka wamtimue mgeni huyo asiyejulikana, lakini akakataa katakata. Pamoja na kutishwa kuwa atatengwa na kijiji, bado msichana huyo alisimama na msimamo wake ule ule wa kumsaidia kwa sababu alikuwa na shida kubwa. Matokeo ya haya, yanamuingiza Siwatu kwenye msukosuko mkubwa ambao hajawahi kuupata kwenye maisha yake kiasi cha kumkatisha tamaa. Fuatilia kisa hiki.

# KAMA IPO, IPO TU-14

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Aliona kabisa kuwa sasa roho yake inakaribia kutoka. Kila kitu sasa alikisikia kwa mbali. Ina maana alikuwa karibuni kuzimia, au kukata roho. Akasikia sauti.

"Basi acha, tuangalie kama amekufa au bado, halafu kama hajafa tummalizie kabisa." Aliisikia sauti hiyo kama yupo kwenye ndoto.

"Haya tangulieni kwenye gari, mimi nammalizia." Akaamuru kiongozi wao. Bado Sam aliliona tukio hilo kama ndoto.

Alijua sasa aliyebaki anachofanya ni kummalizia kwa risasi. Ni kwa sababu alikuwa ameishika mkononi.

Kwa mbali alisikia mlio wa risasi na papo hapo akazirai. Ukawa mwisho wa kusikia chochote kilichopo duniani.

**********************************

"Mpaje kuna kitu nimekiona." Ilikuwa ni sauti ya Siwatu mara baada ya kutembelewa na wifi yake, mpenzi wa kaka yake Dibwela.

"Nini?"

"Hiki kitambaa, nimekiona chini ya kitanda. Hakuna mtu aliyewahi kuingia chumbani kwangu na kukisahau kitambaa hiki."

"Mmh, mwenzangu, wala sijui, lakini wewe si ulikuwa na Bakari ulikuwa unakaa naye inawezekana alikisahau."

"Hapana, leso zake nazijua, siyo hizi, hii kwanza ni aina ya peke yake, Bakari hawezi kuwa na kitambaa kama hiki yenye picha ya mmea wa bangi ambao ni haramu."

"Sasa ni nani Siwatu?"


"Mimi nina wasiwasi kuwa yule mtu aliyekuja kunibaka ndiye aliyeangusha leso hii hapa."

"Inawezekana, sasa cha kufanya peleka ushahidi kwenye ofisi ya kijiji ili atafutwe mwenye kitambaa hicho."

"Hapana Mpaje, kumbuka kijiji kimeshasema kuwa Bakari ndiye aliyenibaka, kitu ambacho si kweli. Bakari nilikuwa nalala naye chumba kimoja, hajawahi hata kunitongoza. Alikuwa ananiheshimu sana kama dada yake kwa sababu ile ya kumuokoa kwenye kifo, sasa kweli hata ukiwapelekea si watasema kuwa ni cha Bakari."

"Sasa utakifanyaje?" Mpaje akauliza.

"Nitamuonyesha kaka Dibwela, yeye anaweza kuwa na cha kufanya, lakini huu ni ushahidi unaoonyesha




**"Siyo hivyo Mpaje, lakini nikisema nilipokiona na kijiji hiki kikijua, mimi naweza kuwa hatarini, naweza hata kuuawa."**

kuwa aliyenifanyia kitendo kile ndiye mwenye leso hii, aliiangusha kwa bahati mbaya."

"Hodi." Walisikia sauti. Ilikuwa ni ya kike. Hawakushtuka kwa sababu walijua ni nani.

"Pita mlango uko wazi."

Aliyeingia ni Mage. "Hamjambo shoga zangu?" Akawasalimia.

Walimuitikia. Lakini aliwakuta wapo kwenye mazungumzo, hivyo ilibidi wawe kimya kidogo.

"Sasa Dibwela atakuwa anapita nacho na kuuliza ni cha nani?" Mpaje akaendelea na mazungumzo.

"Sijui atafanya nini, lakini ndiye nitakayempa siyo mwenyekiti."

"Nini kwani?" Mage aliingilia mazungumzo.

"Hiki kitambaa." Siwatu akamuonyesha.

Mage alionekana kushtuka kukiona. Mshtuko ambao ulikuwa bayana na kuwafanya Siwatu na Mage wahisi jambo.

"Vipi mwenzetu mbona umeshtuka, unamjua nini mwenye kitambaa hiki?" Mpaje alimuuliza kwa sauti ya mshangao.

Mage alibaki kimya kwa muda. Sura yake ilionyesha mshangao uliochanganyikana na woga.

"Mmekipata wapi hiki?" Akauliza kwa woga.

"Ngoja nikwambie Mage, hii leso nimeiokota chini ya kitanda changu. Ilikuwa imeangukia upande wa ukuta chini ndipo nilipokiokota. Sijawahi kukiona kitambaa kama hiki. Lakini kwa sababu niliwahi kuingiliwa na mtu akanibaka, nina wasiwasi kuwa huyu mwenye kitambaa ndiyo mhusika. Sasa ninachotaka kufanya ni kumpa kaka yangu Dibwela, Mpaje amenishauri nipeleke kwa Mwenyekiti wa Kijiji, lakini nimetokea kutokumuamini kabisa, anaweza kukipoteza hiki ushahidi ukakosekana, maana wao hawajafanya uchunguzi wao sawa sawa, wakasema aliyenibaka ni Bakari, wakati mimi mwenyewe najua si kweli."

Bado Mage alikaa kimya akimsikiliza Siwatu.

"Tuambie basi mwenzetu kwa sababu umekishangaa sana, au ulikuwa unashangaa hiyo picha ya mmea wa bangi kwenye leso?"

"Hapana mpaje, mimi... hicho kitambaa nimeshawahi kukiona sehemu."

Jibu hilo lilionekana kuwashtua Mpaje na mwenzake Siwatu.

"Wapi" Mpaje akauliza.

"Mhh mwenzangu, nisije kuonekana mmbea bure."

"Sikiliza Mage, sisi hapa wote ni wanawake. Tusaidiane na kukomesha tabia za namna hii hapa kijijini. Yaani mwanamke anabakwa halafu unaonekana ushahidi, wewe mwenzetu unataka ufunike kwa manufaa ya wanaume kweli?" Mpaje akampa vipande vyake.

"Siyo hivyo Mpaje, lakini nikisema nilipokiona na kijiji hiki kikijua, mimi naweza kuwa hatarini, naweza hata kuuawa."

"Kuuawa?" Siwatu akadakia. "Ina maana kitambaa hiki kina kitu kikubwa sana hadi wewe ukisema ulipokiona unauawa?"

"Ni kweli Siwatu, mimi nikisema tu nipo hatarini, naweza kupotezwa. Kwa sababu wewe angalia, Serikali ya Kijiji imesema aliyekubaka ni Bakari, halafu mimi nikisema kuwa nimekiona sehemu fulani kwa kina fulani, nitaonekana muongo na mchonganishi." Mage aliongea kwa sauti ambayo ilionekana bado imejawa na hofu.

"Haya wewe hutaki kusema, utatusaidia nini kwa hili?"

"Sina la kusaidia Mpaje. Na siyo kwamba sitaki kusema, au sitaki kusaidia kama mwanamke mwenzangu, lakini mimi nahofia usalama wangu."

"Sasa sikiliza Mage, hapa tupo watatu tu, mimi Mpaje na wewe, tulishane yamini kuwa siri hii itabaki humu humu ndani Haitotoka nje."

"Nitaamini vipi? Kwa sababu wewe hicho kitambaa utampa Dibwela, ataanza kupita nacho. Na wanaokijua wanaweza kumwambia ni cha fulani. Itaanza kutafutwa ni nani wa kwanza aliyefichua hilo, nitaonekana mimi, jamani mnataka mnitie matatizoni tu." Akalalamika.

"Nisikilize Mage, sitaki kukuingiza kwenye mkumbo au watu ambao wameshiriki kwenye mpango wa kufanikisha mtu yule kunibaka, lakini mimi nitakachofanya sasa ni kwamba sitamuonyesha hata kaka Dibwela. Kitakaa humu humu ndani. Ninachotaka nijue tu ulikiona wapi? Na inaweza ikawa ni cha nani? Ili tu mimi nijue na wala siendi kumshtaki popote kwa ajili ya kukulinda wewe. Ninachotaka nijue tu."

"Sawa mimi nimekubali, lakini zingatieni mwenzangu, nisije nikalishwa nzi wa puani bure."

"Wala mwaya, hatukusemi. Ya humu yatabaki humu humu bibie." Mpaje akamhakikishia.

"Hicho kitambaa sijui leso, mimi nimeshawahi kumuona nayo Maiko."

Mshtuko mkubwa ukawakumba Siwatu na Mpaje, ingawa kwa Siwatu ulikuwa mkubwa zaidi.

"Maiko huyu huyu ambaye alikuwa ananitaka akasema anataka hadi kunioa?" Siwatu akauliza kwa mshangao.

"Ndiyo huyu huyu mama. Hicho kitambaa mimi nakijua, nimeshawahi kumuona nacho si mara moja au mbili."

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# CHAMA, KAGERE WAAHIDI FURAHA SIMBA 2022/2023

**Na Shufaa Lyimo**

KIUNGO wa Simba Mzambia, Clatous Chama amesema anatarajia kurejea katika ubora wake kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara unaotarajiwa kuanza Agosti 17, mwaka huu pamoja na mashindano ya kimataifa watakayoshiriki.

Akizungumza na gazeti hili muda mfupi kabla ya kuanza safari kuelekea Misri juzi, Chama alisema msimu uliopita timu yake haikufanya vizuri hivyo kwa kushirikiana na wachezaji wenzake wanajipanga kuhakikisha wanatwaa ubingwa.

Chama alisema wamedhamiria kurekebisha makosa yote waliyoyafanya msimu uliopita ili kurejesha furaha katika klabu hiyo.

"Msimu ujao tunarudi upya baada ya kupoteza ubingwa katika msimu uliomalizika, Simba ni timu kubwa hivyo tutashirikiana kitimu kurekebisha makosa yote tuliyoyafanya ili turudishe hadhi ya timu yetu," alisema Chama.

Kiungo huyo alisema sasa hivi yuko fiti baada ya kukaa muda mrefu bila kuonekana uwanjani na anaamini kambi ya Misri itaimarisha kiwango chake na kurejea kwenye soka la ushindani.

"Sasa hivi nipo fiti na ninaendelea vizuri, ninaamini nitakwenda kufanya vizuri kwenye kambi yetu ambayo tunakwenda kuiweka Misri, ninaomba mashabiki pamoja na wapenzi wa Simba waendelee kuniamini bado nipo," Chama alisema.

Aliongeza hawezi kuahidi kuipa mafanikio timu yeye peke yake lakini kwa ushirikiano wa pamoja na wachezaji wenzake watafikia malengo wanayoyahitaji. Alieleza msimu uliopita ulikuwa mgumu lakini msimu ujao unatarajiwa kuwa mgumu zaidi kutokana na timu zote zilivyofanya usajili mzuri wakiwamo watani zao, Yanga.

"Msimu ujao utakuwa mgumu zaidi kwa sababu ninaona aina ya wachezaji wanaosajiliwa ni wachezaji wenye viwango vya juu, vilevile na ofa zilizotolewa na wadhamini zinaifanya kila timu ipambane kusaka matokeo chanya," alisema nyota huyo.

Naye mshambuliaji, Meddie Kagere alisema bado ana uwezo wa kuisaidia Simba kurejesha mataji waliyoyapoteza msimu uliopita.

"Mimi bado ni mchezaji wa Simba, maneno ya mtaani yalikuwa mengi, ninawaahidi mashabiki wetu tunakwenda Misri kujipanga upya, kujiimarisha ili turejee na kasi yetu iliyozoeleka, tunataka kufanya vizuri katika Ligi Kuu na mashindano ya kimataifa," Kagere alisema.

Mnyarwanda huyo aliongeza licha ya ushindani wa namba kuonekana kuwa mkubwa katika kikosi chao, ataendelea kupambana kuhakikisha anapata namba mara kwa mara ili kufikia malengo ya kuipa mafanikio Simba.



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya Ufukweni wakifanya mazoezi ya kujiandaa na mechi ya raundi ya kwanza ya kufuzu fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika dhidi ya Malawi itakayochezwa Julai 23, mwaka huu na marudiano kufanyika Agosti 7, mwaka huu hapa nchini. **PICHA: TFF**

# ZFF yafungua usajili Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

DIRISHA la usajili na uhamisho wa wachezaji kwa ajili ya msimu mpya wa 2022/2023 visiwani Zanzibar limefunguliwa rasmi jana na litafungwa ifikapo Agosti 20, mwaka huu, imeelezwa.

Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi Zanzibar, Hashim Salum aliliambia gazeti hili timu zote zinatakiwa kufanya usajili wake kwa kufuata kalenda hiyo na kuacha kusubiri muda wa nyongeza.

Salum alisema msimu huu bodi hiyo haitakuwa na muda wa kuongeza baada ya muda uliopangwa wa kufunga dirisha hilo la uhamisho na usajili utakapofikia.

Kiongozi huyo amezikumbusha timu zote kufanya usajili kwa kufuata kanuni za mashindano ya msimu huu ili kuepuka migogoro ya usajili wa wachezaji hasa wale ambao bado mikataba.

"Kuna baadhi ya vilabu vinaelewa taratibu za usajili, lakini kuna vingine vinaelewa ila vinafanya makusudi kusajili na kuanzisha migogoro ikiwamo kusajili kinguvu wachezaji bila ya ridhaa ya timu anayotoka, bodi inawataka viongozi hawa waache kusababisha migogoro, wasajili kwa kanuni ili muda wa usajili uwe mfupi na mwepesi kama tulivyopanga," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza timu zote zinatakiwa kusajili wachezaji wake kupita mfumo wa mtandao kama ilivyoelekezwa na Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF).

## Mwiru kuelekea Madola Julai 23

**Na Shufaa Lyimo**

MSHIRIKI pekee wa Tanzania wa mchezo wa kunyanyua vitu vizito kwa upande wa watu wenye ulemavu, Yohana Mwiru anatarajia kuondoka nchini Julai 23, mwaka huu kwenda Ujerumani kwa ajili ya kushiriki michezo ya Jumuiya ya Madola itakayofanyika kuanzia Julai 28 hadi Agosti 8, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jijini jana, mchezaji huyo alisema anaendelea vyema na mazoezi kwa ajili ya kwenda kufanya vizuri katika michuano hiyo.

"Maandalizi yanaendelea vizuri, nimekaa kambini katika nchi tofauti tofauti ambazo nilikutana na walimu wengi, nimejifunza vitu vingi, ninaamini nitakwenda kuipeperusha vyema bendera ya Tanzania," alisema Mwiru.

Nyota huyo alisema anafahamu ushindani utakuwa mkubwa katika mashindano hayo kutokana na washiriki wenzake kutoka mataifa mengine.

Aliishukuru serikali kwa kusaidia gharama za kambi ya muda mrefu ya miezi minne ambayo haijawahi kutokea ili kuwaimarisha wachezaji wanaoshiriki michuani hiyo.

## Wachezaji Kabbadi waomba msaada

**Na Shufaa Lyimo**

NAHODHA wa Timu ya Taifa ya Kabbadi ya wanaume, Joseph Lusinde alisema kikosi chao kimejipanga vizuri kwenda kuiwakilisha nchi katika mashindano ya Afrika yatakayofanyika kuanzia Julai 22 hadi 28, mwaka huu Misri.

Lusinde alisema wamefanya mazoezi mazuri na wanaahidi watarejea nyumbani na medali.

Naye Zuhura Waziri, ambaye ni nahodha wa timu ya wanawake alisema wanaomba wadau mbalimbali wawasaidie ili kufanikisha safari yao.

"Tumejipanga vizuri, ila tunaomba serikali itusaidie tuweze kusafiri, tunaamini tutakwenda kufanya vizuri," alisema Waziri.

Kaimu balozi wa India, Mano Verma ambaye alitembelea kambi ya timu hiyo jana aliwataka wachezaji hao kwenda kufanya vizuri na kupata tiketi ya kushiriki mashindano ya dunia.

Naye Ofisa Michezo wa Baraza la Michezo Tanzania (BMT), Alex Alen alisema anaishukuru serikali ya India kwa namna wanavyojitoa kuisaidia timu hiyo.

## ZISIKUPITE

### DE JONG AIKATAA UNITED
WAKALA wa Frenkie de Jong ameiambia Manchester United kiungo huyo wa kati wa Timu ya Taifa ya Uholanzi mwenye umri wa miaka 25, yuko tayari kuondoka Barcelona, lakini hataki kuhamia Old Trafford. ***(Sport)***

### BARCA YAMBANA DE JONG
BARCELONA wamemwambia Frenkie de Jong kuwa wanataka aondoke katika klabu hiyo na kujiunga na Manchester United. ***(The Athletic)***

### RONALDO ATAKIWA BAYERN
NYOTA wa Manchester United, Cristiano Ronaldo anatazamiwa kukataa ofa nono ya kujiunga na klabu moja ya Saudi Arabia, huku Bayern Munich na Atletico Madrid zikimhitaji mshambuliaji huyo wa Ureno mwenye umri wa miaka 37. ***(ESPN)***

### MAGALHAES ANUKIA JUVE
KLABU ya Juventus wamewasiliana na Arsenal kuhusu kumsajili mlinzi wa Brazil, Gabriel Magalhaes mwenye umri wa miaka 24, kuchukua nafasi ya mlinzi wa Uholanzi, Matthijs de Ligt (22), ambaye anatarajiwa kujiunga na Bayern Munich. ***(Independent)***

### SPENCE KUTUA SPURS
MLINZI wa kulia wa wachezaji wa chini ya miaka 21 wa England, Djed Spence anatarajiwa kukamilisha uhamisho wake wa muda mrefu kutoka Middlesbrough hadi Tottenham Hotspur kwa ada ya takriban pauni milioni 12 ikiwa imekubaliwa. ***(Times)***

### CHUKWUEMEKA ATAJWA BARCA
KLABU ya Barcelona imehusishwa na kutaka kumnunua kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya England chini ya miaka 19, Carney Chukwuemeka ambaye amebakiza mwaka mmoja katika mkataba wake na Aston Villa. ***(Mundo Deportivo)***

### ARSENAL YAMTAKA ZINCHENKO
ARSENAL wanashughulikia mpango wa kumsajili beki wa kushoto wa Timu ya Taifa ya Ukraine, Oleksandr Zinchenko mwenye umri wa miaka 25, kutoka Manchester City. ***(Athletic)***

### GOMEZ ATAKIWA EPL
KLABU ya Arsenal pia inatafuta chaguo la kumsajili beki wa kushoto wa Timu ya Taifa ya Hispania, Sergio Gomez mwenye umri wa miaka 21 kutoka Anderlecht.

### KALIMUENDO SOKONI
LEEDS United wanakaribia kuafikiana kuhusu mkataba wa euro milioni 25 na Paris St-Germain ili kumsajili mshambuliaji Mfaransa, Arnaud Kalimuendo mwenye umri wa miaka 20. ***(90min).***

### BRANTHWAITE KUTUA PSV
MLINZI wa Everton, Jarrad Branthwaite mwenye umri wa miaka 20, atajiunga na PSV Eindhoven kwa mkopo wa msimu mzima. ***(Guardian)***

### BASSEY AGEUKA LULU
KLABU ya Ajax wametoa ofa kwa mlinzi wa Rangers wa Timu ya Taifa ya Nigeria, Calvin Bassey mwenye umri wa miaka 22, huku klabu za Ligi Kuu England zikiwamo Brighton zikiwa na nia ya kutaka kumnunua. ***(Mail)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO AIKATAA TIMU YA WAARABU

Licha ya kutaka kumlipa dau nono Mreno huyo asema hayuko tayari...

**LONDON, England**

CRISTIANO Ronaldo amekataa ofa ya mkataba mkubwa wenye thamani ya euro milioni 275 kutoka kwa klabu ambayo haijatajwa jina ya nchini Saudi Arabia.

Ronaldo amekuwa akihusishwa sana na kutaka kuondoka Manchester United msimu huu wa joto, huku Chelsea ikiaminika ndio wanaopewa nafasi kubwa ya kumsajili fowadi huyo.

90min iliripoti Alhamisi, The Blues sasa wameamua kutomfuata Ronaldo licha ya mmiliki mpya, Todd Boehly kuvutiwa naye.

Kwa mujibu wa ESPN, klabu ya hivi punde zaidi kutaka kumsajili mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or ni klabu ambayo haijatajwa kutoka Saudi Arabia.

Klabu hiyo inasemekana kuwasilisha dau la euro milioni 30 kwa huduma ya Ronaldo, na pia kumpa mchezaji huyo mkataba wa kushangaza ambao ungemfanya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37 kulipwa euro milioni 275 kwa miaka miwili pekee.

Ofa hiyo imekataliwa na Ronaldo, ambaye sasa anaonekana na uwezekano mkubwa zaidi wa kusalia Manchester United baada ya dirisha hili la usajili la majira ya joto.

Mshambulizi huyo alijiunga tena na Mashetani Wekundu msimu uliopita wa joto, na ingawa alifunga mabao 24 katika mashindano yote wakati wa kampeni za 2021/22, klabu hiyo ilipambana na kumaliza nafasi ya sita.

Mambo yanaonekana kuwa ya matumaini zaidi kabla ya msimu ujao, huku Manchester United wakimteua Erik ten Hag mwenye sifa ya juu kama kocha wao mpya.

BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,014,8

MECHI KALI
PYRAMIDS
VERSUS
AL AHLY CAIRO
1 | 3.11
X | 3.16
2 | 2.29

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KLOPP: LIVERPOOL HAITASAJILI KIUNGO



**LIVERPOOL, England**

KOCHA, Jurgen Klopp amekanusha Liverpool inahitaji kusajili kiungo, akifichua anatarajia, Harvey Elliott kuwa "kama mchezaji mpya" msimu huu.

Wekundu hao mapema katika dirisha la uhamisho wa wachezaji waliwasajili Darwin Nunez, Fabio Carvalho na Calvin Ramsey.

Sadio Mane, Neco Williams na Takumi Minamino ni miongoni mwa nyota walioihama klabu hiyo.

Liverpool tangu wakati huo imekuwa ikihusishwa na kiungo, huku Youri Tielemans na Jude Bellingham wakiwa miongoni mwa majina yaliyotajwa, lakini akizungumza kabla ya mechi ya kirafiki ya kujiandaa na msimu mpya dhidi ya Crystal Palace, Klopp alikataa kusajili zaidi msimu huu.

"Hatuwezi kuongeza tu viungo. Tunaheshimu mikataba na wachezaji wetu pia, hiyo inamaanisha mradi tu tumewasaini watapata msaada wetu wote - katika mazoezi, kati ya vipindi, wakati wa michezo na kati ya michezo.

"Hiyo ndiyo hali tuliyo nayo; kwa kweli, unaweza kuhesabu viungo wetu. Na, kwangu, Harvey Elliott ni mchezaji mpya pia, baada ya msimu uliopita jinsi alivyoanza. Yeye ni mdogo sana, alirudi na kipaji, kisha alikuwa na kidogo chini, hiyo ni kawaida kabisa baada ya kuwa nje kwa muda mrefu. Kwa hivyo, nilifurahi sana kumuona."

Klopp pia alionyesha kufadhaika kwake kuhusu ukosefu wa uvumilivu walio nao baadhi ya mashabiki wa soka wa kisasa.

# Lukaku : Nilikosea kurudi Chelsea

**MILAN, Italia**

ROMELU Lukaku amekiri kuondoka Inter Milan na kujiunga na Chelsea kwa mara ya pili lilikuwa ni kosa.

Mwaka mbaya wa Mbelgiji huyo huko Stamford Bridge umefikia kilele chake kwa kurejea Inter Milan kwa mkataba wa mkopo wa msimu mzima, ambapo mchezaji huyo alifurahia kipindi cha mafanikio cha misimu miwili.

Lukaku alirejea Chelsea kwa ada ya pauni milioni 97.5 na hakuwa na wakati mzuri kiuchezaji chini ya kocha, Thomas Tuchel.

Katika mahojiano ya hivi karibuni aliyoonyesha majuto juu ya jinsi ya kuondoka kwake Inter.

"Unajua, niliondoka, lilikuwa kosa kubwa kwangu katika maisha ya soka. Sikutakiwa kuondoka. Tunachofanya kwenye vyumba vya kubadilishia nguo na uwanjani, mahusiano tuliyo nayo sisi kwa sisi, hiyo ni muhimu sana ... ni sawa kwa watu kuona timu yetu imeungana kweli.

"Inter imenipa nafasi ya kucheza kwa kiwango cha juu katika kipaji changu, nimefurahi sana kuvaa jezi hii, tunatarajia kuendelea kukua kama miaka ya nyuma. Tunapaswa kuendelea hivi ikiwa tunataka kufikia lengo."



372,576/-

SUPA JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 16/07/22 | 21:30 | Magdeburg vs Fortuna Dusseldorf | 3.03 | 3.37 | 2.28 |
| 02. 16/07/22 | 22:00 | AL Asyooti Sport vs Al Ahly Cairo | 3.16 | 3.16 | 2.29 |
| 03. 16/07/22 | 22:30 | Atletico Pr vs Internacional | 2.35 | 3.28 | 2.99 |
| 04. 16/07/22 | 22:30 | Sampaio MA vs Vasco da Gama | 2.87 | 3.01 | 2.57 |
| 05. 17/07/22 | 00:00 | Newell'S Old Boys vs Racing Club | 2.82 | 3.18 | 2.62 |
| 06. 17/07/22 | 00:30 | Guarani SP vs Bahia BA | 3.07 | 2.97 | 2.45 |
| 07. 17/07/22 | 01:00 | Avai vs Santos | 2.89 | 3.08 | 2.54 |
| 08. 17/07/22 | 03:00 | Ceara CE vs Corinthians | 2.40 | 2.99 | 3.19 |
| 09. 17/07/22 | 12:00 | Machida Zelvia vs V Varen Nagasaki | 2.47 | 3.10 | 3.00 |
| 10. 17/07/22 | 12:30 | Ryukyu vs Omiya Ardija | 3.14 | 3.24 | 2.31 |
| 11. 17/07/22 | 14:30 | Hansa vs Heidenheim | 2.45 | 3.29 | 2.84 |
| 12. 17/07/22 | 16:00 | Wisla Plock vs Lechia Gdansk | 2.76 | 3.30 | 2.44 |
| 13. 17/07/226 | 17:30 | Servette Geneva vs St. Gallen | 2.34 | 3.74 | 2.69 |
| 14. 17/07/22 | 19:00 | Union Santa Fe vs Huracan | 2.76 | 3.06 | 2.76 |
| 15. 17/07/22 | 19:30 | EL Gouna FC vs Talaea El Gaish | 3.18 | 2.78 | 2.53 |
| 16. 17/07/22 | 22:00 | Nautico PE vs Chapecoense | 2.46 | 3.01 | 3.01 |
| 17. 17/07/22 | 22:00 | Arab Contractors vs Ceramica Cleopatra | 3.03 | 2.78 | 2.63 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 16/07/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 1284 | Jahn Regensburg vs SV Darmstadt | 3.50 | 3.70 | 1.91 |
| 14:00 | 3453 | Tottenham vs Sevilla FC | 2.15 | 3.33 | 2.99 |
| 14:00 | 4133 | St. Pauli vs Nurnberg | 2.31 | 3.45 | 2.80 |
| 15:00 | 1460 | CSKA Moscow vs Ural Yekaterinburg | 1.60 | 3.79 | 5.18 |
| 15:00 | 2895 | Viimsi JK vs Ida-Virumaa FC Alliance | 1.39 | 5.24 | 6.25 |
| 15:15 | 3112 | Kuala Lumpur vs FC Petaling Jaya City | 1.47 | 4.13 | 5.70 |
| 16:00 | 2067 | Skovde Aik vs IK Brage | 2.51 | 3.42 | 2.71 |
| 16:00 | 2512 | Norrkoping vs Malmo | 3.10 | 3.29 | 2.11 |
| 16:00 | 2793 | Dalkurd FF vs Orebro SK | 2.74 | 3.51 | 2.44 |
| 16:00 | 4945 | Vitebsk vs Neman Grodno | 4.24 | 3.20 | 1.81 |
| 16:00 | 5905 | Selangor FC vs Penang | 1.46 | 4.33 | 5.51 |
| 17:00 | 1458 | Jerv vs Sandefjord | 2.37 | 3.42 | 2.77 |
| 17:00 | 2366 | HJK Helsinki vs VPS Vaasa | 1.44 | 4.12 | 6.09 |
| 17:00 | 3652 | Nomme Kalju vs Trans Narva | 1.28 | 5.29 | 7.63 |
| 17:00 | 3799 | Valmiera Fk/Bjss vs BFC Daugavpils | 1.09 | 7.67 | 18.68 |
| 17:30 | 3532 | Gazovik Orenburg vs Kryliya Sovetov | 2.55 | 3.30 | 2.60 |
| 18:00 | 1374 | Torpedo Zhodino vs Isloch | 2.37 | 3.13 | 2.78 |
| 18:00 | 3815 | Ostersunds vs Osters IF | 4.18 | 3.62 | 1.84 |
| 18:00 | 3938 | FK Igman Konjic vs Siroki Brijeg | 2.51 | 2.95 | 2.76 |
| 18:00 | 5500 | AL Salt vs Moghayer AL Sarhan | 2.45 | 3.19 | 2.65 |
| 18:30 | 1643 | Domzale vs NK Celje | 2.45 | 3.40 | 2.51 |
| 18:30 | 2145 | Lokomotive Sofia vs CSKA Sofia | 3.68 | 3.33 | 1.89 |
| 18:30 | 3301 | IFK Mariehamn vs Hifk | 1.60 | 3.77 | 4.80 |
| 18:30 | 4369 | Jagiellonia vs GKS Piast Gliwice | 2.65 | 3.19 | 2.45 |
| 18:30 | 5134 | Djurgardens IF vs IFK Varnamo | 1.40 | 4.33 | 6.50 |
| 19:00 | 1163 | AC Bellinzona vs Lausanne-Sport | 3.33 | 3.62 | 1.91 |
| 19:00 | 1842 | FS Metta/Lu vs Rigas Futbola Skola | 13.70 | 7.24 | 1.13 |
| 19:00 | 1967 | AS Trencin vs MSK Zilina | 1.93 | 3.73 | 3.19 |
| 19:00 | 2713 | Spartak Trnava vs Zlate Moravce | 1.31 | 4.61 | 8.23 |
| 19:00 | 2955 | Ham-Kam vs Bodo Glimt | 4.11 | 3.76 | 1.77 |
| 19:00 | 3631 | BSC Young Boys vs FC Zurich | 1.55 | 4.50 | 4.80 |
| 19:30 | 1568 | Ghazl EL Mahallah vs Zamalek | 6.04 | 3.47 | 1.61 |
| 19:30 | 4661 | Kuressaare vs Tallinna JK Legion | 1.66 | 3.63 | 4.51 |
| 19:30 | 5062 | Coca Cola vs Ismaily SC | 1.98 | 2.96 | 4.32 |
| 20:00 | 3718 | Akhmat Grozny vs Spartak Moscow | 2.59 | 3.34 | 2.54 |
| 20:00 | 3953 | Dnepr Mogilev vs Slavia Mozyr | 4.92 | 3.94 | 1.56 |
| 21:00 | 3623 | Korona Kielce vs Legia Warszawa | 3.78 | 3.24 | 1.90 |
| 21:00 | 3695 | Backa Topola vs Javor Ivanjica | 1.37 | 4.42 | 6.87 |
| 21:15 | 3910 | Maribor vs NK Radomlje | 1.45 | 4.13 | 5.89 |
| 21:30 | 1279 | Sport Podbrezova vs Slovan Bratislava | 10.76 | 5.28 | 1.22 |
| 21:30 | 5135 | FC Winterthur vs FC Basel | 3.31 | 3.66 | 2.00 |
| 21:30 | 5543 | Longford Town vs Athlone Town | 1.43 | 4.52 | 5.50 |
| 22:00 | 1792 | Pyramids vs Al Ahly Cairo | 3.11 | 3.16 | 2.29 |
| 22:00 | 1924 | HNK Sibenik vs HNK Rijeka | 4.80 | 3.77 | 1.60 |
| 22:00 | 3733 | Finland W vs Germany W | 22.52 | 8.42 | 1.07 |
| 22:00 | 5661 | Denmark W vs Spain W | 10.89 | 5.55 | 1.21 |
| 22:30 | 1551 | Atletico Pr vs Internacional | 2.21 | 3.14 | 3.04 |
| 22:45 | 1162 | Audax Italiano vs Colo Colo | 3.79 | 3.35 | 1.86 |
| 23:00 | 3213 | Llaneros FC vs Atletico Huila | 1.82 | 3.20 | 4.20 |
| 23:30 | 4899 | Univ San Martin vs Universitario | 4.41 | 3.62 | 1.67 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# SINGONE KUFUNGA USAJILI NYOTA WAGENI AZAM FC

**Na Saada Akida**

MABOSI wa Azam FC wamesema usajili wa kumnasa kiungo mkabaji kutoka Ivory Coast, Claude Singone kwa ajili ya kusaidia timu hiyo kufanya vizuri katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika watakayoshiriki utakuwa ni wa mwisho kuelekea msimu mpya.

Taarifa zilizopatikana jijini zinasema Singone alionekana akiwa na mmoja wa watendaji wa juu wa klabu hiyo kwa ajili ya kukamilisha usajili wake.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa Azam FC, Thabit Zakaria 'Zakazakazi', alisema baada ya kumtambulisha, James Akaminko kwa kumpa mkataba wa miaka miwili, wako katika mchakato wa kumalizana na nyota mwingine wa kimataifa ambaye hakutaja jina lake.

Zaka alisema wanaendelea kufanya maboresho katika kikosi chao kwa kufuata mapendekezo yaliyotolewa na benchi la ufundi kwa kuzingatia nafasi zote.

"Ujio wa Akaminko utaimarisha zaidi kikosi cha timu yetu kulingana na uwezo wake wa kucheza nafasi nyingi, na tunatarajia kushusha kifaa kingine, tuko katika hatua ya mwisho kumalizana na beki wa kati wa kimataifa, huyu atafunga usajili wetu," alisema Zaka.

Aliongeza baada ya kukamilisha usajili wa beki huyo timu itaingia kambini keshokutwa na Julai 22, mwaka huu wataelekea Misri kwa ajili ya kuweka kambi ya siku 20 ili kujiandaa na msimu mpya.

"Maandalizi ya safari yetu kuelekea Misri yamekamilika, tunatarajia wachezaji wetu wataimarika na kurejea nchini wakiwa na kasi na tayari kwa ajili ya kupambana, timu zote zimefanya usajili mzuri, hivyo nasi lazima tukajiwinde," Zaka alisema.

Hadi sasa Azam FC imemamilisha usajili wa wachezaji watano wa kigeni ambao ni golikipa, Ali Ahamada ambaye ni raia wa Comoro, Isah Ndala, Tape Edinho, Kipre Junior, Akaminko na wachezaji wazawa ni pamoja na Nathaniel Chilambo, Cleophance Mkandala na Abdul Suleiman 'Sopu'.

Azam FC ilimaliza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliopita katika nafasi ya tatu nyuma ya mabingwa Yanga na Simba, zote za jijini huku Geita Gold FC ikishika nafasi ya nne na kupata tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.



Kaimu balozi wa India, Mano Verma (kulia), akizungumza na wachezaji wa Timu ya Taifa ya Kabbadi inayojiandaa na mashindano ya Afrika yanayotarajiwa kufanyika kuanzia Julai 22 hadi 29, mwaka huu nchini Misri. **PICHA: SHUFAA LYIMO**

# Geita Gold kusajili Mcameroon

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Geita Gold ambayo msimu ujao itaiwakilisha Tanzania katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika imesema ipo hatua za mwisho za mazungumzo ya kumsajili straika mpya kutoka Cameroon lakini pia ikikaribia kumbakisha mshindi wa kiatu cha dhahabu msimu uliomalizika, George Mpole.

Ofisa Habari wa Geita Gold FC, Samuel Dida alisema wapo katika maboresho ya kikosi kwa kufuata mapendekezo yaliyotolewa na benchi la ufundi ambalo limeweka wazi linahitaji kuongeza wachezaji wapya sita.

Dida alisema kati ya wachezaji hao, tayari wanne wameshapata sahihi zao, lakini kwa sasa hawatawataja majina yao kwa sababu bado wanakamilisha taratibu za kisheria.

Alisema tayari wameshamnasa beki wa kati kutoka Jamhuri wa Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na wakiwa kwenye mazungumzo wa mastraika wawili kutoka Cameroon na Kenya.

"Msimu ujao huenda tukawa na straika wa kigeni kutoka Cameroon au Kenya, tuko kwenye mazungumzo nao, mmoja kati ha yao tutamsajili, lakini tumesajili wachezaji wawili Watanzania na beki mmoja Mkongomani, tunaweka kwanza vizuri mambo ya kisheria kabla ya kuwataja," alisema Dida.

Aliongeza mkataba wa Mpole unaelekea ukingoni na mazungumzo naye yanaendelea vizuri huku nyota huyo akisema anafurahia maisha ya klabu hiyo.

Michezo

Jumamosi Julai 16, 2022

Nipashe



## Ronaldo aikataa timu ya Waarabu




Rais wa Yanga, Injinia Hersi Said (kulia), akiwa na nyota mpya wa Yanga, Stephane Aziz Ki, raia wa Burkina Faso ambaye alitambulishwa rasmi na klabu hiyo usiku wa kuamkia jana jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA: TUTAFANYA MAKUBWA, TULIENI

●●●Yafanikiwa kumbakisha Manula Msimbazi huku hatima ya...

**Na Saada Akida**

KUKIWA na usiri mkubwa ndani Bodi ya Wakurugezi ya Simba, chini ya Mwenyekiti wake, Salim Abdallah 'Try Again', imemwongeza mkataba mpya wa miaka miwili kipa chaguo la kwanza wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Aishi Manula.

Lakini pia klabu hiyo imewataka mashabiki wake kutulia kwa sababu imewaandalia mambo mazuri na makubwa katika msimu mpya.

Manula alikuwa amemaliza mkataba na klabu hiyo na tayari sintofahamu ya hatima yake ilianza kuzua taharuki na sasa mabosi wa Simba wamemalizana na mlinda mlango huyo wa zamani wa Azam FC.

Taarifa za uhakika zilizolifikia gazeti hili zinasema Simba imemalizana na Manula na sasa ataendelea kuwa sehemu ya nyota wanaoitumikia klabu hiyo.

Chanzo hicho kilisema uongozi umejipanga kumpa heshima Manula kwa kuandaa utambulisho unaofanana na thamani yake katika muda muafaka ambao utapangwa.

"Ni kweli Aishi hayuko katika kikosi cha Simba huku Misri, lakini sio kwamba hayuko ndani ya timu hiyo bali yuko katika majukumu ya Stars, akimaliza ataungana na Simba kwa sababu ameshaongeza mkataba wa miaka miwili," kilisema chanzo chetu.

Taarifa zaidi zilisema Manula alitamani kupata timu nje ya Tanzania, lakini tatizo linalokwamisha kuondoka ni ofa ndogo ambazo zinakuja lakini pia hahitaji kwenda kukaa benchi huko atakapotua.

Manula alisema ni kweli mkataba wake na Simba umemalizika na sasa ameweka mbele nguvu na akili kuitumikia Stars.

"Mkataba na Simba umemalizika na bado sijasaini mkataba timu yeyote, ila kama nitaongeza au kusaini sehemu yoyote litawekwa wazi," alisema Manula.

Naye Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally aliwataka wanachama na mashabiki wa klabu hiyo kuwa watulivu na hivi karibuni wataweka wazi majina ya wachezaji ambao wameongezea mikataba na walioachana nao.

Aliongeza zoezi la kutikisa nchi litaendelea kwa kutambulisha wachezaji wao wapya waliowasajili wakiwa kambini Misri.

"Wanasimba wasiwe na presha juu ya usajili, uongozi uko makini kwa wachezaji ambao wanaendelea kubaki katika timu lakini pia kuhakikisha lile zoezi letu la usajili linaendelea kutambulisha mchana kweupe.

"Kuhusu Mhilu (Yusuph), bado anaendelea na mazungumzo na uongozi, na wakifanikisha au kuelewana, basi mustakabali wake ndani ya Simba utawekwa hadharani," Ahmed alisema.

Kiongozi huyo aliongeza hali ya wachezaji wa Simba walioweka kambi Misri iko vizuri na jana jioni walitarajiwa kuanza mazoezi ya kujiwinda na msimu mpya utakaoanza Agosti 17, mwaka huu.

"Timu kubwa kwenye mazingira bora ya kujiandaa kufanya makubwa katika msimu mpya," alisema Ahmed.

## Kambi ya Uturuki Yanga yayeyuka

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kufanikiwa kumsajili winga wa kimataifa raia wa Burkina Faso, Stephane Aziz Ki, kikosi cha Yanga kinatarajia kuweka kambi yake Karatu, Arusha ili kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa watakayoshiriki.

Aziz Ki ambaye alikuwa akiichezea Asec Mimosas, alitambulishwa rasmi usiku wa kuamkia jana baada ya mabosi wa Yanga kukamilisha taratibu za usajili huo.

Ofisa Habari wa Yanga, Haji Manara alisema wale ambao walikuwa wanawabeza kuhusu kuipata saini ya nyota huyo sasa watakuwa wanaona vitendo.

"Kwa wale ambao walikuwa wanabeza kwamba hatuwezi kupata saini ya nyota mwenye uwezo mkubwa na namba 10 bora basi iwafikie kwamba tumempata na tupo naye ndani ya kikosi cha Yanga,".

Wakati huo huo, taarifa zilizopatikana jijini jana zinasema Yanga itaenda kuweka kambi yake Karatu baada ya safari ya kwenda Uturuki kuota mbawa.

## Stars hesabu kali ikiiwinda Somalia

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Kim Poulsen amesema amewafuatilia kwa karibu wapinzani wao Somalia na kuongeza hawatawadharau pale watakapokutana katika mchezo wa kusaka tiketi ya kufuzu fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa wachezaji wa ndani (CHAN).

Somalia inayotumia Uwanja wa Benjamin Mkapa itaikaribisha Taifa Stars Julai 23, mwaka huu na timu hizo zitarudiana kwenye uwanja huo baada ya wiki moja.

Poulsen alisema kikosi chake kitafanya maandalizi mazuri na kuhakikisha wachezaji wanakuwa makini kwa sababu Somalia ni timu nzuri na imeimarisha benchi lake la ufundi kwa kuajiri kocha mpya.

"Tunalazimika kushinda mchezo huo wa kwanza, Somalia sio wabaya ni timu nzuri na hatutawadharau," alisema Kim.

Aliongeza kufanya vizuri katika mchezo hiyo ya CHAN, itawasaidia kujiandaa na mchezo wa kusaka tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), dhidi ya Uganda utakaochezwa Septemba, mwaka huu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >